ANAYENG'ANG'ANIA

Hebu tuendelee tu kusimama kwa muda kidogo kabla hatujaketi. Na tuombe kwanza. Nami nashangaa, usiku wa leo, kwenye usiku wa pili wa mkutano, ni haja ngapi zilizoko, mngependa . . . zijulikane kwa mkono ulioinuliwa, "Mungu, sikia ombi langu." Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

2 Baba yetu wa Mbinguni, tunakujia Wewe tena, usiku wa leo, usichoke kamwe kusikiliza wito wa watoto Wako, daima uko tayari kujibu, tukiomba jambo moja tu, kwamba tutaamini kwamba tunapokea kile tunachoomba. Tunaomba, Bwana, ya kwamba utaondoa kila uvuli wa shaka, usiku wa leo, kwa Roho Wako Mtakatifu mkuu katika Neno Lako, tunaomba kwamba utajibu kila haja. Nasi tunajua ya kwamba tunapata haja yetu, kwa sababu tunamwamini Yeye aliyeahidi jambo hilo.

3 Na sasa, Baba wa Mbinguni, tunaomba ya kwamba utawaokoa wenye dhambi, uwaponye wagonjwa, uliimarishe Kanisa, ujipatie Mwenyewe utukufu. Nisaidie usiku wa leo, Bwana, ili nipate kuwa chombo kitakachotumiwa na Mungu. Msaidie kila mtu hapa, kwamba watakuwa vivyo hivyo. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

4 Mwaweza kuketi. Naona watu wakiweka leso sasa jukwaani, hapa, juu ya mimbara, hasa, kwa . . . zipate kuombewa. Tunaamini katika hilo. Hiyo ni mojawapo ya huduma zetu kuu, ni kuombea leso na kadhalika, kwa ajili ya—ya wagonjwa na wanaoteseka. Tunaamini ya kwamba ni Maandiko, tunaamini ya kwamba hiyo ndiyo amri. Mfano: Paulo aliombea leso na nguo, akawapelekea wagonjwa, nao wakaponywa.

5 Nakumbuka wakati mmoja, huko Afrika Kusini, nilikuwa na . . . Niliona katika . . . Ninaamini hiyo picha iko kwenye kitabu ambapo tulikuwa na ninii kubwa mno, kile tunachokiita, magunia ya turubai, hapa Marekani, yamejaa tu barua za siku moja za leso pekee, maelfu kadhaa yazo. Nami nilikuwa nikiziombea, ndipo mwandishi wa habari akasema, "Ndugu Branham ni mshirikina sana, huombea—huombea leso." Inaonyesha tu jinsi watu, wasiojua Maandiko, ni dha—ni dhana ya kimwili jinsi gani wanaweza kuwa nayo juu ya kazi ya Mungu, mnaona, wakati hawalijui.

6 Nilikuwa Rumi, nilikuwa huko chini, na nikitazama . . . ambapo msanii wa Kiyunani alikuwa amepaka rangi dha—dhana ya . . . Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni. Na ni dhana ya jinsi gani, jamani! Hawa alionekana kama namna fulani ya mnyama wa zamani za kale, naye Adamu, sijawahi kuona kitu kama hicho maishani mwangu. Inaonyesha tu kile ambacho nia ya kimwili inaweza kuchora, wakati haijaongoka

kwa utukufu wa Mungu. Ninaamini Hawa alikuwa ndiye mwanamke mrembo zaidi aliyepata kuishi duniani, hiyo ni kweli, kwa sababu aliumbwa mpya na mikono ya Mungu, bila kuguswa na dhambi yoyote. Adamu, mtu mkamilifu zaidi ambaye angaliweza kuishi, nje ya Kristo maana Yeye alikuwa ni Adamu wa pili, mtu mkamilifu zaidi.

7 Lakini nia ya kimwili inaweza kutoa wazo kwamba alikuwa na kichwa kikubwa *hivi*, na bega moja limeinuka, na lingine limeshuka, naye Hawa mguu mmoja mdogo, na huo mwingine mkubwa mno, na, loo, nywele zikining'inia chini, mdomo wake umeenda kombo. Vema, jamani, nisingeweza kuwaza Roho Mtakatifu akifanya kitu kama hicho. Lakini, inaonyesha nia ya kimwili inapoingia ndani yake.

8 Hivyo ndivyo akili zetu zitakavyoendelea vivyo hivyo, tukiziacha ziondoke kwenye Neno la Mungu katika dhana hizo za kimwili. Binti yangu, hapa usiku wa leo, alisema leo, alikuwa akijaribu kunichezea, anasema, "Ninayo *Elimuadili ya Darwin* hapa, ningependa uisome, Baba."

9 Nikasema, "Asante, nilifanya hivyo miaka kadhaa iliyopita, mara moja ya hicho inatosha." Lakini Biblia hii ya kale, kamwe hatutosheki nayo, tunaimiminia ndani tu kwa utukufu wa Mungu.

10 Samahani kwamba kanisa zima, asubuhi ya leo, halingeweza kuwa kwenye kifungua kinywa chetu. Ni ushirika mzuri jinsi gani tuliokuwa nao! Roho Mtakatifu mbarikiwa alitutembelea na kutupa Ujumbe ambao . . . Loo, ulikuwa ni wakati mzuri sana wa ushirika katika mambo ya Mungu.

11 Nami najua niliwachelewesha kidogo jana usiku, nami, labda, ninachoka kidogo. Huu ni mkutano wangu wa tisa mfululizo, nami nina likizo ndogo baada ya mikutano miwili zaidi. Lakini nitajaribu kuwaachilia mapema kidogo usiku wa leo, kwa sababu najua ninyi ni watu mnaofanya kazi, inawabidi kurudi kazini mwenu, wala sininii . . . wala sitaki kuwaweka.

12 Lakini nina furaha kuona hata umati umeongezeka, usiku wa leo, inaonyesha shauku. Na marafiki, hilo ni zuri sana leo, kwa sababu sote tunajua, inatubidi tu kujua hili: Uamsho umekwisha. Tunajua kwamba, mioto inawaka kidogo, nayo shauku ya watu inaisha.

13 Mnaona, tulikuwa na uamsho, uliodumu kwa miaka mingi. Historia inaonyesha kwamba m—mtu, mwinjilisti, kwa kawaida sehemu zake bora zaidi ni miaka yake mitatu ya mwanzoni, na baada ya hapo anaishia sifa ya yale aliyohubiri katika miaka hiyo mitatu. Halafu, uamsho hauchukui muda mrefu sana, lakini huu umekuwa ukiendelea kwa miaka kumi na mitano hivi, kwa maana ndio uamsho wa mwisho, naamini, nasi tuko moja kwa moja kwenye wakati wa mwisho. Ninaamini huo mwingine utakuwa ni kulivuta Kanisa, Wateule, kutoka kwenye makundi

na kuwakusanya pamoja, nalo hilo litaondoka, na kwa hiyo, tunatazamia hilo litukie.

14 Lakini tunaweza kuona mioto ya uamsho ikipungua, shauku za watu, kila mtu amechoka, anaenda kulala, shauku imekwisha. Na kuona shauku kama hii miongoni mwa watu, ina-. . . inanichangamsha, na kujua kwamba bado kuna moto unaowaka huku kote Oregon. Mungu awabariki daima. Hebu na tuupepee usiku wa leo kwa bidii tu tuwezavyo kwa Neno. Nalo Neno, unapolipepea, litazaa Roho Mtakatifu, Upepo wenye Nguvu Uendao Kasi ambao utauwasha moto tena. Mungu atujalie.

15 Na sasa, ili kuhifadhi wakati. . . Ninyi ni wazuri sana kuzungumzia. Ningeweza kuzungumza nanyi kwa saa kadhaa, lakini si—sina budi tu kuwa mwangalifu na kuhifadhi wakati huu. Katika dakika chache, baada ya kumaliza kuongea, nitaziombea hizi. . . juu ya leso hizi, nanyi sikuzote mmekaribishwa kuzileta, tunafurahia kulifanya.

16 Sasa, tunawatakeni, mfungue, usiku wa leo, muhtasari fulani nilio nao hapa, kwa njia ya—ya maskini. . . Kile ninachoninii. . . ninachotaka kufanya, ninachojaribu kufanya, si siri, ni kujaribu kujenga imani ndani ya watu, kufikia ambapo tunaweza kuwa na upeo mkuu, na jambo fulani litukie kweli ambalo litaitikisa nchi nzima.

17 Sasa, tulifanya hivyo, kwa neema ya Mungu, kule Grass Valley, ambapo hapakuwa na mtu mmoja dhaifu aliyesalia katikati ya hilo kusanyiko lote, jumba hilo kubwa la mikutano, hakukuwako hata na mmoja. Sikuwaombea wagonjwa, niliendelea tu kujenga imani, nikaendelea tu na Neno, katika urahisi wa Neno, kwa njia rahisi niliyo nayo ya kulielezea. Lakini watu walilishikilia tu na kukaa moja kwa moja, na ndipo ule wakati mkuu ukawadia, na, loo, kila kitu humo jengoni kikainuliwa.

18 Na ilikuwa hivyo tena huko Spokane, hivi majuzi usiku, wakati sehemu yote ya mbele ilikuwa imejaa viti vya magurudumu, na wagonjwa kwenye machela, na vitu kama hivyo, ndipo kabisa kupitia kwenye safu hiyo Roho Mtakatifu akashuka, akimkomboa kila mmoja wakati tu akimfikia, moja kwa moja namna *hiyo*. Hapo. . . Walilala hapo kwenye viti hivyo vya magurudumu na kutoa jasho na kila kitu, wakisikiliza, wakishikilia imani hiyo, wakiishika tu, na kuchunguza, na kutafuta kujua. Ndipo baada ya kitambo kidogo, mara Roho Mtakatifu akashuka moja kwa moja chini, akashuka moja kwa moja kwenye safu namna *hiyo*, na kila mmoja wao akainuka akaenda zake. Mnaona, mnaona?

19 Shida ni kwamba, sisi watu, tuna haraka kupindukia, haina budi kufanywa sasa hivi, hamwezi kurudi tena. Mnaona? Ndipo unapoliweka hilo akilini mwako, unaona, kwamba, utapoteza papo hapo. Uko—uko kwenye misingi ya kupoteza papo hapo,

hu—huna cha kusimamia. Huna budi kuwa na subira, "Wale wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya, watapanda juu kwa mbawa kama tai." Na—napenda hilo. Iweni tu na subira, ngojeni.

20 Mungu hana haraka. Aliwaacha wana wa Kiebrania watembee moja kwa moja kwenye ile tanuru ya moto kabla hajafanya chochote, hiyo ni kweli, akamwacha Danieli aingie moja kwa moja kwenye tundu la simba, akamwacha Yesu aingie moja kwa moja kaburini, nayo Nafsi Yake ikashuka kuzimuni, ndipo akamfufua moja kwa moja kupitia mashimo yasiyo na mwisho, moja kwa moja kupitia kaburini, na kukata kila njia ya ibilisi, na kuingia moja kwa moja Utukufuni pamoja Naye. Mnaona? Hakika. Yeye hana haraka, Yeye ni Mungu. Mnaona? Ananinii tu. . . Sisi tunakuwa tu na pupa, ndilo jambo pekee, mnaona, tunalikosa.

21 Kwa hivyo usiwe na haraka, subiri, tazama, sikiliza. Chukua Maandiko, yachunguze, uone kama ni kweli, na kama ni kweli, lishikilie, kama sivyo, niambie ili niweze kulirekebisha. Kwa hiyo tu—tunaona kama. . . Kila kazi lazima iwe ni kazi ya Roho Mtakatifu. Lazima iwe ni kazi Yake, ni Yake. Na lazima itoke kwenye Biblia. Hatupaswi kutoa chochote kutoka kwenye dhana au hoja fulani, lazima tuitoe kutoka kwenye Biblia.

22 Bwana akipenda, nataka kuzungumza usiku mmoja, kabla sijaondoka, juu ya *Wakati Mashariki Na Magharibi Zinapokutana*. Nimekuwa nikijaribu huku na huko pwani kuingiza hilo. Natumai nitalipata kabla sijaondoka hapa, *Wakati Mashariki Na Magharibi Zinapokutana*. Na halafu, Bwana akipenda, ningetaka kuzungumza wakati mmoja juu ya *Neno La Mungu Lililoimarishwa*, na Bwana akipenda.

23 Nilikuwa nikitazama kule, katika moja ya. . . mkoba wangu, leo, nami ninawazia masomo madogo, ya kadhalika, ya kanda ambazo zimenaswa, takriban mahubiri mia tano ama jumbe ambazo Bwana amenipa, kutoka katika Neno Lake, kuyaweka. Na halafu, usiku wa leo, kuja jukwaani inahitaji maombi na kusoma. Nafikiri mtu yeyote anapaswa kujificha ndani. . . kutoka kwenye. . . chumba chake cha kusomea katika upya wa Mungu kukutana na kusanyiko.

24 Mara nyingi nimeshangaa ningefanya nini kama nilikuwa na matone mawili ya Damu halisi ya Yesu Kristo kwenye—kwenye sinia, bilauri. Jinsi ningetembea nayo kwa uangalifu sana kuhakikisha sikuimwaga! Lakini mnajua, usiku wa leo, machoni Pake, nina kilicho kikubwa zaidi mkononi mwangu, walionunuliwa kwa Damu Yake. Alimwaga Damu Yake kwa ajili yako, kwa hiyo nifanyeje na hawa? Mnaona, ni jukumu kubwa, nikijua ya kwamba itanibidi kujibu kwenye Siku ya Hukumu kwa kila neno. Na kwa hivyo, basi hebu tulikaribie kwa kicho kabisa.

25 Fungueni Biblia zenu sasa, ili tuweze kusoma baadhi ya Neno Lake. Maneno yangu yatashindwa, kwa sababu ni neno la mwanadamu, Maneno Yake hayatashindwa kamwe. Kwa hiyo kusoma tu Neno . . . Hebu na tufungue Mathayo mlango wa 15 na tuanzie kwenye kifungu cha 21, tafadhalini.

> *Yesu akaondoka huko, akaenda kando pande za Tiro* ya *Sidoni.*
>
> *Na, tazama, mwanamke Mkananayo wa* mipaka *ile, akatokea, akampazia sauti, akisema, Unirehemu, Bwana, Mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa sana na pepo.*
>
> *Wala yeye hakumjibu neno. Nao wanafunzi Wake wakamwendea, wakamwomba, wakisema, Mwache aende zake; kwa maana anapiga kelele nyuma yetu.*
>
> *Akajibu, akasema, Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.*
>
> *Naye akaja akamsujudia, akisema, Bwana nisaidie.*
>
> *Akajibu, akasema, Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.*
>
> *. . . akasema, Ndiyo, Bwana, lakini hata mbwa hula . . . makombo yaangukayo mezani pa bwana zao.*
>
> *Ndipo Yesu akajibu, akamwambia, Mama, imani yako ni kubwa: na iwe kwako kama utakavyo. Akapona binti yake tangu saa ile.*

26 Ninataka kuchukua, ama kutoa somo kutoka kwa hilo, kama nikiliita hivyo, kwa kama dakika thelathini, kunena. Ninataka kuchukua neno moja ambalo ningependa kutumia kujenga ninii . . . muktadha kwake, na hilo ni neno la *Anayeng'ang'ania.* Sasa, *anayeng'ang'ania* ni kuninii . . . linamaanisha "kuendelea kushikilia." Webster inasema ni ku—kushikilia, kushikilia katika kuweka lengo, kuendelea kushikilia yale ufanyayo.

27 Watu wa nyakati zote, walio na imani katika kile wanachojaribu kufanikisha, wamekuwa waking'ang'ania. Inakubidi kung'ang'ania, huwezi kuketi tu kitako na kusema, "Kweli, nitaona kile Joe atakachofanya juu yake." Huwezi kufanya hivyo. Na kabla ya kung'ang'ania, lazima uwe na imani katika kile unachojaribu kufanikisha, na iwapo huna imani, basi hutang'ang'ania.

28 Sasa, watu katika nyakati zote wamejaribu jambo hilo, lakini . . . na wamekuwa wa kung'ang'ania. Lakini kile ulicho nacho . . . Kung'ang'ania, kwanza, ni kuwa na imani, halafu basi unapaswa kujua chanzo cha imani yako.

29 Sasa, watu wengi wameng'ang'ania jambo baya, na daima wametokea vibaya. Nimrodi alitaka kujenga mnara, aling'ang'ania, lakini hakuweza kuumaliza. Nebukadneza

alitaka mji usiopatikana na mauti, lakini kamwe haku—hakufanikiwa. Lakini mnaona, ninyi . . . jambo la kwanza unalopaswa kufanya, kung'ang'ania, ni kujiweka uwe sawa na mkweli.

30 Siku moja rafiki yangu wa thamani, daktari, alikuja nyumbani kwangu, mtu mzuri sana. Ukitaka kumwandikia kuhusu hili, jina ni Dk. Sam Adair, pembeni mwa Ukuta, Barabara ya Maple, au, Barabara ya Ukuta na Soko, Jeffersonville, Indiana; anayo kliniki. Rafiki msiri wangu sana, tulikuwa wavulana wa shule moja, mmoja wa madaktari bora sana tulio nao ma—mashariki.

31 Nayo nyumba ilikuwa imejaa watu wanoombewa. Nao watu wakiingia, jinsi wanavyoingia kutoka kila mahali kuombewa! Ndipo mke wangu akarudi, naye akasema, "Billy, Dk. Adair yupo hapa."

Nikasema, "Mweke kwenye chumba cha kusomea. Tuna watu katika vyumba hivi vingine ambao . . . Mweke kwenye chumba cha kusomea, nitakuwa naye haraka niwezavyo."

32 Na kulikuwako na mtu pale, kutoka Kanisa la Kibaptisti la Barabara ya Walnut huko Louisville, aliye na kansa kwenye wengu. Nao walimfanyia upasuaji huu, haukufanikiwa, naye huyo mtu alikuwa yuafa. Naye akaokolewa na kuponywa hiyo kansa. Nami nilikuwa nikimshughulikia, wakati huo, kuona yale Bwana angeniambia kumhusu.

33 Kwa hiyo basi, tulipoingia kumwona maskini Dk. Sam, alikuwa ameketi mle ndani amekunja mikono yake, mtu mzuri tu sana. Alikuwa, vema, huyo daktari alikuwa amemleta Billy Paul, na mwanangu, na kadhalika, tulikuwa marafiki wazuri sana, alikula nyumbani kwangu na kadhalika, tulikuwa tu marafiki wa karibu sana.

34 Naye akasema, "Bill, nataka kukuuliza jambo fulani." Sasa, tunafahamiana vizuri vya kutosha hata sina haja ya kumwita "Daktari," Nilimwita tu "Sam," naye huniita "Bill." Na kwa hiyo akasema, "Bill, nataka kukuuliza jambo fulani." Kasema, "Una maoni gani kuhusu mji huu, hivi huoni unahitaji kliniki?"

Nami nikasema, "Hakika, mji wowote unahitaji kliniki, madaktari wazuri."

Akasema, "Naam, naamini mji huu unaihitaji."

Nikasema, "Nami pia, Sam."

Naye akasema, "Vema," akasema, "unafikiri ninastahili ku—kuwa na—kuwa na kliniki hii?"

Nami nikasema, "Je, unaliwazia?"

Akasema, "Naam."

35 Nikasema, "Sijui daktari mwingine yeyote ambaye ni afadhali niseme kwamba—kwamba nilifikiri anastahili kuwa

nayo." Sasa, yeye ni mkali, maskini jamaa mgumu, lakini yeye ni . . . Sikuzote nilimwita kobe, yeye ni mwororo kwa ndani, lakini ni mgumu kwa nje, ni ganda tu anamojirudishia ndani. Mungu anaujua moyo wa mwanadamu. Kila mtu angalisema Sauli wa Tarso alikuwa mtu mgumu pia, lakini Mungu aliujua moyo wake. Kanisa lilimchagua Mathiya, lakini tuligundua ya kwamba Mungu alimchukua Sauli, maskini huyo Myahudi mwenye pua ya ndoano, hasira kali . . . hakuwa kitu, kumfanya kitu fulani.

36 Sasa, na kwa hiyo mtu huyu akasema, "Vema, nataka kliniki hii." Ndipo kasema, "Unajua, Bill, kwamba mimi—mimi ni . . . Nataka kumtumikia Bwana," akasema, "lakini mimi ni mbaya sana."

Nikasema, "Loo, sijui kuhusu hilo."

37 Akasema, "Lakini mimi na—najaribu, katika kazi yangu, kufanya niwezalo kwa Bwana." Akasema, "Mimi—mimi—mimi . . . Baadhi ya watu hao weusi wanakuja," kasema, "wanahitaji upasuaji, nao hawana pesa." Kasema, "Unajua ninawafanyia upasuaji." Na hiyo ni kweli. Mtu yeyote asiye na pesa, anaendelea, anafanya hiyo kazi kwa vyovyote vile. Yeye ni daktari mashuhuri wa upasuaji.

Nami nikasema, "Naam, loo, na—naamini hilo."

Akasema, "Nataka kukuuliza kitu." Kasema, "Je, waweza kumwomba Bwana kwa ajili yangu?"

Nami nikasema, "Naam, hakika."

Akasema, "Nina ninii kidogo . . ." Kasema, "Je, unafikiri kliniki hiyo inapaswa kujengwa wapi?"

38 Nikasema, "Sijui." Nikasema, "Kama wewe . . ." Rudi nyuma sehemu nyingine, hiyo ni nchi ya mafuriko, nao walijenga ukuta wa mafuriko. Nikasema, "Ningepata upande huu wa ukuta wa mafuriko."

Akasema, "Naam."

Nikasema, "Vema, kuna mengi, mahali pakubwa hapa kwenye kona *fulani*."

Akasema, "Vema," akasema, "mzishi amekwisha kupachukua mahali hapo, wanajenga kituo cha mazishi."

Nami nikasema, "Vema," Nikasema, "basi vipi huko chini mahali ile Kampuni ya Mafuta ya Pfau ilipokuwa?"

39 Akasema, "Hiyo imechukuliwa, watajenga mahali pa aiskrimu huko." Akasema, "Nina mahali pazuri sana, Bill," lakini akasema, "mtu fulani alipanunua kabla yangu," kasema, "mwanamke mkongwe huko Kentucky." Kasema, "Ni pale ambapo shule ya zamani ya idara ilipokuwa hapa chini."

40 Kisha kasema, "Najua mzee mmoja kidogo anampenda." Ndipo kasema, "Unajua nini? Ninaamini kama ningeweza

kumpa yapata dola mia tatu, nawe ungeninii . . . " Kasema, "Nami . . . Aliinunua kwa dola elfu sita." Kasema, "Nitampa kama dola mia tatu ku—kusudi aniuzie, kisha nitampa kumi kwa ajili yake."

41 Nami nikasema, "Sasa, Sam, angalia hapa, humpi Mungu rushwa kwa chochote." Nikasema, "Iwapo utazungumza na Mungu, hatuna budi kuliweka papa hapa vizuri, hakuna hongo kwake hata kidogo." Nikasema, "Kamwe hatuwezi kufanya hivyo na Mungu."

Akasema, "Vema, sikulimaanisha hivyo, Bill. Lakini hiyo ni ploti nzuri sana."

Nikasema, "Vipi . . . Kwa nini usifanye hivi? Hebu tuikabidhi tu kwa Mungu tuone Mungu atasema nini juu yake."

Akasema, "Sawa."

42 Nikasema, "Vema, toka kitini ugeuke." Kwa hivyo akafanya hivyo, ndipo tu—tukapiga magoti pale na kuomba kwa muda kidogo. Tulimngoja Bwana kama dakika kumi na tano, ishirini, baada ya muda mfupi ono likatokea.

43 Nikasema, "Daktari, simama." Nikasema, "Umepata neema kwa Mungu. Utajenga ma—mahali pako, kliniki yako. Litakuwa jengo refu, litajengwa kwa tofali nyekundu, dari fupi, na karibu litachukua bloku moja ya mji." Naye akanitazama kigeni sana. Nami nikasema, "Haitakuwa kwenye ile shule ya idara, sahau hilo. Itajengwa pembeni mwa Barabara ya Ukuta na Soko, ambapo nyumba ile kubwa ya kale imekaa nyuma ya kile kilima."

44 Akasema, "Hebu kidogo, Bill." Akasema, "Nakumbuka ukiniambia kuhusu Bill Hall." Sina wakati wa kuingia katika hilo . . . Alimkatia tamaa kuwa atakufa kwa kansa, tayari imekula ini lake, na wataalamu wote wamesimama karibu. Nami, nikienda kuwinda kuchakulo asubuhi hiyo, niliangalia, nikaona ono la Bw. Hall, Nikaenda nikampigia simu, nikasema, "Bw. Hall ataishi."

Akasema, "Itabidi maskini huyo daktari mzee aone hilo."

Anaishi usiku wa leo, akihubiri katika Kanisa la Kibaptisti la Milltown.

45 Kwa hivyo, akasema, "Ninajua kuhusu Will Hall na mambo haya yote." Lakini kasema, "Bill, nimetoka kotini hivi punde juu ya mahali hapo." Kasema, "Huko Philadelphia, mwenye hiyo mali anaishi huko, na kuna kitu kuihusu kwamba haiwezi kuguswa kwa miaka ishirini na mitano."

Nikasema, "Daktari, uliwahi kunisikia nikikwambia jambo lolote katika Jina la Bwana ambalo halikuwa hivyo?"

Akasema, "Lakini Bill, hiyo—hiyo . . . " Kasema, "Sitaki kukushuku."

46 Nikasema, "Hunishuku mimi, unamshuku Yeye." Nikasema, "Bwana amekupa mahali hapo. Sasa, asingefanya hivyo, kama tayari hakuwa amelifanya, mnaona, huku wewe unafanya hivyo." Lakini nikasema, "Tayari amekupa mahali, kliniki hiyo itakuwepo." Akajikuna kichwa, akatoka nje, hakusema lolote.

Kesho yake asubuhi, mke wangu anayeketi hapo angeshuhudia, alinipigia simu, akasema, "Bill."

Nikasema, "Kitu gani?"

Akasema, "Ninaganda hadi kufa." Na ilikuwa yapata wakati huu mwakani, kuna joto sana Indiana.

Nikasema, "Kuna nini, daktari?"

47 Akasema, "Unajua, walifanya mkutano, jana usiku, huko Philadelphia, na tayari nimeinunua ploti hiyo." Akasema, "Ni mali yangu, na kliniki inajengwa." Hiyo hapo imesimama leo. Akasema, "Kama mtu yeyote, wakati wowote, atatilia shaka jambo lolote, waambie wanipigie simu." Mnaona, na hiyo ni mahali popote, mnaona.

48 Na jinsi hilo lilivyo, lakini mnaona, maskini jamaa huyo aling'ang'ania. A—a—alitaka kujenga kliniki, ilikuwa moyoni mwake. Naye akaja, huku akiwa ni mshiriki vuguvugu tu wa kanisa, bali akaja akimtafuta Mungu. Sasa, hiyo ndiyo njia ya kupata jibu, mtafute Mungu.

49 Daktari mmoja alikuwa ameketi pamoja naye siku moja, naye akasema, "Loo, ninaamini kuna kitu kama uponyaji wa Kiungu," lakini akasema, "liko akilini tu."

Nikasema, "La, la."

Akasema, "Ninaamini kama mtu angeamini kwamba anaweza kwenda kugusa nguzo, angepona."

50 Nikasema, "Bwana, ni nani angeweza kuwa na imani katika kugusa nguzo? Huna budi kuwa na . . . Imani si legevu kamwe, haina budi kutegemezwa kwenye kitu fulani cha kimsingi."

51 Mwanamume anapomchukua mke wake, hana budi kuweka imani yake kwa mwanamke huyo, naye mke hana budi kuweka imani yake kwa mwanamume huyo, sababu fulani ya kufanya lengo la maisha, ikiwa hana, basi kuna kasoro, na haitafanikiwa. Huna budi kuwa na imani. Na ni nini kilicho bora kuamini kuliko Neno la Mungu?

52 Kama maskini yule mtu mweusi wa kusini alivyosema, alisema, "Afadhali niwe nimesimama juu ya Neno la Mungu kuliko kusimama Mbinguni."

Kasema, "Kwa nini, Mose?"

53 Akasema, "Mbona, mbingu na nchi zitapita, lakini Neno halitapita." Kwa hivyo anataka- . . . alitaka kuwa huko kweli, hakika. Kwa hivyo hiyo ni sawa kabisa. Biblia ilisema katika Ufunuo 21 . . . "Mbingu na nchi zitapita, lakini ninii Langu—

lakini Neno Langu halitapita kamwe." Alisema yeye. . . katika Ufunuo 21, aliona mbingu mpya na nchi mpya, kwa maana mbingu za kwanza na nchi zilikuwa zimepita. Yesu alisema mbingu na nchi zote zitapita, lakini Neno Lake halipaswi.

54 Sasa, hatuna budi kuwa na imani ya msingi juu ya kile tunachofanya. Hivyo ndivyo jinsi hasa maono hayo yanavyoweza kutimizwa, ni kwa sababu yamewekewa msingi juu ya ahadi ya Kristo. Na kama Malaika huyo wa Bwana, Nguzo hiyo ya Moto, ambayo mna picha Yake hapa (Ambayo nafikiri wamekuwa nayo hapa juu, sivyo?), kama Hiyo haikusema sawasawa na Neno hili, nisingeiamini. Sijali jinsi lilivyoonekana kuwa halisi, halina budi kuja kulingana na Neno hili.

55 Naye huyo Malaika wa Bwana Ndiye, ile Nguzo ya Moto iliyowafuata Israeli, ama, Israeli waliifuata, hasa, kupitia nyikani, kisha ikafanyika mwili na kukaa miongoni mwetu. Mnaamini hivyo, sivyo? Hakika. Mungu alikuwa ndani ya Kristo.

56 Alisema, "Nalitoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu." Hiyo ni kweli? Baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, na kupaa Kwake, Sauli wa Tarso alikuwa akienda zake Dameski, na mara hiyo Nguzo kubwa ya Moto, ya Nuru, mbele yake ikampiga machoni, naye akaanguka chini. Ndipo akasikia Sauti ikisema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?"

Akasema, "U nani Wewe, Bwana?"

57 Akasema, "Mimi ni Yesu." Alikuwa amerudi kwa Mungu. Aliingia gerezani, kama Nuru, iliyomtoa Petro gerezani, ikamtoa nje.

58 Na sasa, kama huyo ni Malaika wa Bwana akiwaongoza watu hawa, Yeye atafanya jambo lile lile alilofanya wakati alipodhihirishwa katika Mwana wa kweli wa Mungu, atafanya vivyo hivyo katika wana wa Mungu wenye mamlaka, kwa maana Yesu alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Kama Uzima Wake uko ndani yetu, utazaa yale yale; na kama anafanya mambo kinyume na Maandiko, basi haiwezi kuwa ni Malaika yeye yule.

59 Lakini kama akitoa Maisha yale yale aliyokuwa alipokuwa hapa duniani, akidhihirishwa katika mwili, na huku aliahidi kudhihirishwa tena, vivyo hivyo, basi ni Roho yeye yule, Mungu yeye yule, kwa Neno lile lile. Mnaona ninachomaanisha? Sasa, basi unaweza kuweka imani yako kuwa hiyo ni kweli. Na katika makumi ya maelfu ya maono kote ulimwenguni, nitamwomba mtu yeyote wakati wowote anionyeshe pale lilipowahi kushindwa, halishindwi, na haliwezi kushindwa.

60 Hili, mnaloliona hapa, ni ono dogo, ni mambo madogo tu. Unafanya hivyo wewe mwenyewe, ni wewe. Mwangalie Kristo, Yeye alikuwa ni Utimilifu wa Mungu. Mungu aliishi ndani ya Kristo bila kipimo, alikuwa na Roho bila kipimo, tunaye kwa kipimo. Lakini kama nina kijiko kimoja cha maji kutoka kwenye

ziwa nje hapa, ama, baharini, hayo ndiyo yaliyokuwamo ndani ya Kristo, kama nina kijiko kimoja cha maji, kiwe tu kijiko cha maji kutoka kwake, lakini kemikali zile zile zilizoko katika bahari nzima ziko kwenye kijiko hicho, sio tu . . . si—si nyingi sana, lakini kemikali zile zile.

61 Na kama tuna Roho wa Mungu ndani yetu, ni kazi zile zile na Roho yeye yule, madhihirisho yale yale. Mnaona? Ni ninii tu . . . Ndipo unaweka imani yako juu ya hilo, nawe unapoona ni nini, basi unaweza kung'ang'ania, unajua unaposimama.

62 Kama . . . kama—kama ishirini . . . Kama nilikuwa nafa kwa njaa, na mtu anipe m—mkate, uh, senti ishirini na tano zingenunua mkate, na mtu anipe thamani ya kununua mkate, ambayo ni senti ishirini na tano, ninaweza kushangilia niwezavyo nikiwa na robo hiyo mkononi mwangu kadiri ninavyoweza nikiwa na mkate mkononi mwangu, kwa sababu nina ushahidi kwamba nitaishi. Nina senti ishirini na tano, uwezo wa kununua, mkononi mwangu.

63 Na wakati mwanamume ama mwanamke anapoiona imetia nanga ndani yao, wana imani, wanaweza kushangilia. Sijali mkono wako unasema nini, au jinsi unavyoumwa, endelea kuamini, unang'ang'ania. Wewe—wewe—wewe ni—wewe ni—wewe unang'ang'ania, hakuna kitakachokuzuia, unayo. Sijali, madaktari elfu kumi wangeweza kusimama, waseme unakufa, ungewacheka tu, utembee juu yake. Naam. Kama kwe- . . . Na itatendeka. Lakini unaona, watu wengi *wanatumaini* tu, na *wanatamani*, na kadhalika, inakuwa dhaifu, loo, dhaifu, sana, sana, unapoanza kunena kuhusu masharti ya imani.

64 Watu wengi, tumefundishwa, weka mikono juu ya wagonjwa, na hilo ni sawa. Lakini mnaona, ninachojaribu kujenga *hapa* ni, hutalazimika kusema, "Ndugu Branham aliniwekea mikono." "Nilikuwa Mbele za Yesu Kristo, nilimgusa. Ndugu Branham hakuwa na uhusiano wowote nalo, hakuna mtu mwingine aliyekuwa na uhusiano wowote nalo . . . Mungu alifanya hivyo."

65 Nami nitawaambia hili, ndugu, kama litawahi kufanywa, itabidi Mungu alifanye. Hiyo—hiyo ni kweli. Ninawatakeni mliamini, mliamini, na kisha mng'ang'anie, mshikilie.

66 Na watu mashuhuri ambao wameomba . . . George Washington, huko katika Bonde la Forge, aling'ang'ania sana. Aliomba usiku kucha wakati Waingereza walikuwa ng'ambo ya pili. Ndipo kesho yake asubuhi, haijalishi . . . Hapo walisimama askari wetu wa Marekani, nusu yao hawakuwa na viatu miguuni, askari wa Marekani bila viatu miguuni.

67 Washington aliomba mpaka akalowa maji hadi kiunoni mwake, mpaka akapata jibu kutoka Mbinguni. Ndipo mto unaoenda kasi kesho yake asubuhi (Bonde la Forge), haukumsumbua, akavuka, aling'ang'ania, kama askari wake walikuwa na viatu au la, kama upinzani ulikuwa mkubwa

au la. Risasi tatu za gobori zilipitia kwenye koti lake wala hazikumgusa kamwe. Kwa nini? Alikuwa ameomba mpaka akamshika Mungu. Hakuna gobori, hakuna jeshi, hakuna mto, hakuna magumu, chochote kile, anaendelea.

68 Kama vile Yoshua na Kalebu, wakati hao . . . wengine wote wa hilo kabila walisema, "Loo, hatuwezi kuiteka. Hatuwezi kuiteka. Loo, tunaonekana kama panzi, wao ni majitu."

69 Lakini Yoshua aling'ang'ania, kwa maana alijua Mungu alisema, "Nawapa ninyi." Mnaona, walikuwa wakiangalia yale waliyoweza kuona, Yoshua alikuwa akiangalia aliyosema Mungu. Hilo ndilo . . . Inategemea kile unachoangalia. Mkristo huangalia yasiyoonekana, yasiyoonekana. Silaha zote za Ukristo hazionekani, kitu cha milele hakionekani. Vitu vinavyoonekana ni vya kawaida, nayo ardhi ndiyo mama ya hayo yote.

70 Lakini yasiyoonekana, silaha zote za Mungu, ni mambo yasiyoonekana, upendo, furaha, amani, imani, uvumilivu, fadhili, upole, unyenyekevu, kadhalika, Mungu, Roho Mtakatifu, Roho. Yote yasiyoonekana, hayo ndiyo mambo ya kudumu, mambo ya Milele, hayo ndiyo silaha zetu zote.

71 Kila kitu ambacho Mkristo anaweza kutegemea ni kile kisichoonekana, ahadi ya Mungu. Nasi tunaangalia kitu ambacho hatuoni kwa macho yetu. Jambo lingine, kuliona kwa macho yako, hulioni; *kuona* maana yake "kulielewa." Ukiangalia kitu chochote moja kwa moja, useme, "sikioni," unamaanisha hukielewi. Ukielewa . . . Kitu fulani kina ufahamu ya kwamba Mungu ametoa ahadi Yake, na Kitu fulani kimekugusa hata ukaamini, huko ni kuelewa kwamba ahadi ya Mungu ni kwa ajili yako, ndipo jambo fulani litatukia. Basi sijali, hakuna mtu ulimwenguni anayeweza kukuzungumzia akakuondoa kwake, uko njiani basi, hakuna kitakachokuzuia.

72 Washington, alipoomba kabisa, alikuwa tayari. Wakati watu wanaposikia kutoka kwa Mungu na kujua kwamba ni ya Kimaandiko, basi wanaweza kung'ang'ania. Nuhu, mkulima tu, mtu . . . Unaona, u—ukoo wa—wa watoto wa Kaini walikuwa werevu, wanasayansi wakuu, mafanikio makubwa katika sayansi, tunayafuata hayo. Lakini wana wa Sethi walikuwa wanyenyekevu, wakulima wadogo, wakulima, wafuga kondoo, na kadhalika. Mungu daima huishi katika unyenyekevu.

73 Shida yake leo, ni kwamba sisi Wamarekani, daima tunatafuta kitu kikubwa na kiangavu, naye Mungu hafanyi hivyo, kitu chenye kelele. Mungu anaweza kuteka maji mengi zaidi kwa jua katika dakika tano kuliko tunayoweza kupampu kwa pampu yenye kelele katika siku arobaini. Hakika. Lakini tunatafuta kitu kikubwa na chenye kelele, Mungu anatafuta kitu ambacho ni kidogo na cha kimya.

74 Upepo unaoenda kasi, ngurumo, moshi, tetemeko la ardhi, hakuna hata kimoja cha vitu hivyo kilichomvutia nabii Eliya

alipokuwa pangoni, lakini aliposikia ile Sauti ndogo tulivu, Mungu alikuwa mle ndani, ndipo akaja akitembea, hakuna kimoja cha hayo mengine kingeweza kumvutia. Ni jambo fulani mle halina budi kutia nanga, jambo fulani halina budi kutukia.

75 Nuhu, aling'ang'ania sana baada ya kusikia Sauti ya Mungu kujenga safina. Ungeweza kuwazia hiyo i—ilikuwa ni siku ya jinsi gani? Ungeweza kuwazia upinzani aliokabiliana nao, wakati walipokuwa na ustaarabu mkubwa zaidi kuliko tulio nao sasa? Walijenga piramidi, tusingeweza kuzijenga; walijenga Sfiniksi, inabeba mabehewa kumi na sita, kuuwekelea mguu, tusingeweza kuijenga, bado hatuna nguvu za utenda kazi kufanya hivyo, lakini walikuwa nazo. Wangeweza—wangeweza kuupaka mwili dawa usioze, kutengeneza mumiani ambayo ingeonekana kuwa ya kawaida hata leo, tusingeweza kufanya hivyo. Walikuwa na rangi ambayo hatukuwa nayo, mafanikio mengi walikuwa nayo.

76 Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Angalieni mle ndani sasa, walikuwa—walikuwa werevu, lakini Nuhu alikuwa amezungumza na Mungu. Haijalishi ni kiasi gani Ujumbe wa—wake haukuafikiana na mawazo yao ya kisayansi, bado aliendelea kwa sababu alikuwa amemsikia Mungu, akajenga safina vivyo hivyo tu.

77 Hebu tuiangalie kwa muda kidogo, wakati tukiwa kwenye hili somo. Ninaweza kuona wakati ukija, watu wanamcheka, wakisimama karibu kila siku na kumwangalia akizipigilia mbao, yeye na familia yake. Lakini walisema, "Aisee, Nuhu, nataka kukuuliza jambo fulani." Wanasayansi mashuhuri, "Unajua, tunaweza kurusha mwezini kwa rada yetu. Nataka kukuuliza jambo. Nionyeshe mahali ambapo kuna mvua huko angani. Nionyeshe mahali palipo na maji huko juu, hakuna maji huko.

78 "Nuhu, ulisema itamwagika. Sasa, iko wapi hata imwagike? Tunaweza kuthibitisha kisayansi hayapo hata kidogo, kwa vyombo vyetu, hapa, kuthibitishia. Acha, ewe mtu, una—una kichaa, unarukwa na akili. Acha kujenga safina hiyo ya kijinga, shuka uje ukajiunge nasi, sisi wengine. Acha tule, tunywe, na tushangilie."

79 Lakini Nuhu alikuwa amemsikia Mungu. Naye akasema, "Sijali kama vyombo vyenu vinaonyesha hakuna kitu huko, ikiwa Mungu alisema itakuwa huko, anaweza kuiweka huko." Aling'ang'ania. Akaweka ukingo wa juu wa hiyo mashua, na kutengeneza pa—pande zote, na kuiandaa. Alipomaliza kuijenga, alisimama mlangoni mwa hiyo safina na kuhubiri wokovu kwa kuingia tu kwa huo mlango. Wakamcheka.

80 Siku moja akaanza kuona, hawa hapa wakaja simba dume na jike, farasi dume na jike, na wote wakaanza kuingia kwenye

safina. Mungu akasema, “Jitayarishe, Nuhu, nimetosheka na vurugu zao, za kutokuamini kwao. Nitatuma Hukumu niliyoahidi.”

81 Vema, ndugu, dada, nasema hivi, natumai hamfikirii mimi ni mlokole, lakini ninaamini kwamba kurudia huko huko kumekaribia. Mungu amechoshwa na wakati huu wa kisayansi wa kurusha mwezini, kudondosha makombora, tulio ndani yake. Mbona, ni mnara mwingine wa Babeli! Je, hamjui kwamba Mungu ataiharibu dunia hii? Alisema atafanya hivyo.

82 Hiyo ndiyo sababu niko hapa nje, usiku wa leo. Hiyo ndiyo sababu tunajaribu kusonga mbele kupata kila nafsi tuwezayo, kwa maana subira ya Mungu katika siku za Nuhu ni kama ilivyo sasa, hapendi mtu yeyote aangamie. Lakini, naye Mungu alituma kila aina ya karama anayoweza mbele ya watu, na bado wanakaa nje ya Ufalme. Ni kwa sababu mengi yake yanatoka mimbarani, tunajua hivyo, kuzikana siku za miujiza, kumkana Roho Mtakatifu, na kadhalika, ambako kunasababisha jambo hilo.

83 Sasa, tunaona kilichotukia, siku moja Nuhu alipoingia na familia yake, basi naweza kuwasikia wakisema, “Hao hapo maskini wanyama wako wanaovunda, ingia moja kwa moja ndani, ishi nao sasa.” Loo, enzi yao kuu ya kielimu, mnajua, waliyoishi. Na—na kwa hiyo, basi mlango ukafungwa.

84 Kulikuwa na waaminio wakwamia mpakani ambao walikuwa wakihudhuria mkutano wa Nuhu. Vema, kama vile tu ilivyo sasa, watu wanaketi wakati wote kanisani, bali kamwe hawachukui hatua kuja mbele. Wanafurahia kumsikia mchungaji akihubiri na *kadhalika*, lakini hawasongi mbele kamwe. Hivyo basi jambo la kwanza . . . Kamwe hawataki kuingiza mikono yao ndani yake, wasije wakatambulishwa pamoja nalo.

85 Ndugu, loo, ndugu! Loo, nina furaha sana kutambulishwa pamoja nalo! Na—nataka utambulisho wangu, nijue kuwa mimi ni mmoja wao. Heshima kuu sana niliyopata kuwa nayo, kutambulishwa pamoja na watu wanaoitwa wendawazimu kwa sababu ya Injili. Hiyo ni kweli.

86 Sasa, wakati—wakati katika . . . Wakati wa Nuhu ulipowadia kwa ajili ya ile gharika, basi baadhi ya hao waaminio wakwamia mpakani walisema: “Sasa, alikuwa mzee mzuri. Sasa, huenda jambo fulani likatukia, kwa hiyo mbona, niwaambie nini, tutapanda na kusimama kuizunguka safina, ndipo kama kweli mvua ikianza kunyesha, kutoka huko juu, kama alivyosema, ama, maji, mwajua nini? Tutabisha mlango, naye ni mzee mpole, ataturuhusu tuingie.” Naam, lakini si Nuhu aliyeufunga mlango, Mungu ndiye aliyeufunga mlango. Hivyo wao . . .

87 Sasa, mnaona, baada ya kuwa Mkristo, watu wengi wanawazia, “Vema, baada ya kuwa Mkristo, hilo latosha, yote

ninayopaswa kufanya ni kusema tu, 'Vema, utukufu kwa Mungu, kila kitu ni changu.'" La, bwana. Umekosea. Unapigania kila inchi ya ardhi unayochukua.

88 Mungu aliwaambia Israeli, kule Misri, "Ninawapa nchi hiyo ya ahadi." Lakini akamwambia Yoshua, alipoingia mle, "Kila mahali nyayo za miguu yenu zinapokanyaga, hapo nawapa." Walikuwa tayari wamepewa, lakini ilibidi wapiganie kila inchi yake, maneno mengine, nyayo za miguu zilimaanisha umilikaji, endelea tu kutembea. Sasa, iliwabidi kuipigania, bali Mungu alikuwa amewapa.

89 Halafu basi, naye Nuhu, alipoingia na kuketi ndani ya safina, aliingia katika mwezi wa—wa Mei, tarehe kumi na saba Mei, wakati Nuhu alipoingia ndani ya safina, kulingana na Biblia. Sasa, nami ninamsikia akisema . . . Alishuka hapa kwenye orofa ya chini juu ya kuhesabiwa haki, na ilikuwa na vitu vyote vitambaavyo. Akapanda kwenye ghorofa ya pili juu ya utakaso, na ilikuwa ni ndege wote. Bali alienda hadi juu ambapo Nuru ilikuwa ikimulika chini, kwenye ubatizo wa Roho, ndani ya safina. Basi akapanda huko juu, akawaambia jamaa yake yote, kasema, "Sasa, ninyi ketini hapa. Sasa, asubuhi, jua halichomozi, mawingu meusi, kama moshi, yatapasua angani, nayo maji yatakuwa yanamwagika."

90 Lakini kesho yake asubuhi, jua lilichomoza tu kama lilivyowahi kufanya. Ningewazia kulikuwa na masikitiko fulani kuhusu Nuhu, lakini tayari alikuwa amefungiwa ndani. Siku ya pili ikapita, hakuna kilichotokea. Naye akakaa humo siku saba, siku saba, akimjaribu.

91 Kila mwana, kila mtoto amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa. Mungu atashuka katika mkutano, na kuonyesha ishara kuu na maajabu, nanyi mtashangaa, kisha atawajaribu kwake kuona kama kweli mnalimaanisha au la, amina, kuwajaribu aone kama kweli mnaamini au la.

92 Basi alimwacha Nuhu akae pale na kulitolea jasho kwa muda wa siku saba, lakini kwenye asubuhi hiyo ya saba, anga lilikuwa likinguruma na weusi, matone makubwa ya mvua yakaanza kuanguka, mifereji ya maji machafu ikaanza kujaa, na barabara ikainuka, maji ndani yake, juu kabisa, moja kwa moja kwenye safina, ikaelea. Watu wakabisha hodi, lakini ikaendelea mbele zaidi na zaidi, nao waovu wakazama.

93 Nuhu aling'ang'ania kwa sababu alisikia Sauti ya Mungu, naye akashikilia. Ndipo miaka mia moja na ishirini akahubiri Ujumbe, hakudhoofika kamwe, alizidi kuwa na nguvu, alimwamini Mungu, aling'ang'ania.

94 Musa, yule nabii mtoro, alikuwa na elimu yote ambayo ingeweza kushindiliwa ndani yake, kwa sababu alikuwa mwana wa binti Farao. Naye alikuwa na theolojia yote, alikuwa mwerevu sana, angeweza kuwafundisha Wamisri hekima. Na

kwa yote aliyokuwa nayo, pamoja na ufahamu kwamba alizaliwa ninii . . . maisha ya kiroho, au kuwa na—nabii . . .

95 Manabii hawafanywi, manabii wanazaliwa. Manabii . . . Kuna karama ya unabii katika Kanisa, lakini manabii wanazaliwa, wanalo Neno la Bwana.

96 Yesu Kristo alikuwa Mwana wa Mungu kote kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, mnaamini hilo, Mwana-Kondoo. Naye Isaya alimwona Yohana Mbatizaji miaka mia saba na kumi na miwili kabla hajazaliwa, "sauti ya mtu aliaye nyikani." Musa alizaliwa mtoto mzuri. Yeremia, Mungu alisema, "Kabla hata hujachukuliwa mimba tumboni mwa mama yako, nalikujua, na kukuita, na kukutakasa, nikakuweka kuwa nabii wa mataifa." Kabla hajazaliwa kutoka tumboni mwa mama yake, alikuwa na Neno la Bwana tangu utotoni na kuendelea. Hiyo ni . . . Alikuwa nabii.

97 Naye huyu hapa Musa, alijua alikuwa nabii wa Bwana, lakini hakuwa amepata ujuzi huo bado, kitu cha kumfanya ang'ang'anie, alitoroka kwa sababu aligundua kitendo chake cha kijeshi hakikufanya kazi. Ndipo akaingia nyikani, akakaa huko mpaka alipokuwa mzee, umri wa miaka themanini, masharubu yakining'inia chini, na labda kichwa chake chenye upara kilikuwa tayari kimegeuka kahawia kutokana na jua kuangaza, kutokana na kuwachunga kondoo wa Yethro.

98 Basi alikuwa huko nje asubuhi moja, naye akasikia, kisha akatazama juu mlimani, na kulikuwa na kichaka kilichowaka moto, akageuka aone kichaka hiki, ndipo alipokuwa pale, akasikia Sauti ikisema, "Vua viatu vyako."

99 Sasa, vipi kama Musa alisema, "Nitavua tu kofia yangu"? Hiyo haifai kitu. Hiyo ndiyo sababu Biblia ni . . . Ninaamini ya kwamba kila Neno Lake halina budi kutimizwa. "Vua viatu vyako," akavua viatu vyake.

100 Akasema, "MIMI ni Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Nimesikia kuugua kwa watu Wangu. Nakumbuka ahadi Yangu kwa Ibrahimu." Amina. Jinsi nilivyo na furaha Yeye anaikumbuka tena siku hizi, kwamba angeimwaga Roho Yake. "Ninakumbuka ahadi Yangu, nami nitakutuma huko chini ukawakomboe."

101 Naye akatoa udhuru wa kila namna, lakini akasema, "Hakika nitakuwa pamoja nawe." Unajua wakati mwingine basi, kunapotokea jambo kama hilo, unang'ang'ania sana.

102 Naye Musa aling'ang'ania sana. Hakungoja hadi aunde jeshi. Unajua, wakati mwingine, unapong'ang'ania na kusikia Sauti ya Mungu, inakufanya ufanye mambo ya kipuuzi kwa nia ya kimwili, unatenda kigeni, kiajabu, wewe ni mtu wa kipekee. Angalia jinsi Musa alivyotenda kijinga: Kesho yake tunamwona pamoja na mke wake wametagaa juu ya nyumbu, akiwa na Gershomu kwenye nyonga yake, na mzee mwenye masharubu

yaliyoning'inia *hivi*, ndevu zikipepea, na maskini mzee mwenye umri wa miaka themanini, akiwa na fimbo iliyopinda mkononi mwake, akishuka barabarani, "Haleluya! Haleluya!"

"Unaenda wapi, Musa?"

"Nashuka kwenda Misri, kuiteka," uvamizi wa mtu mmoja. Kwa nini? Alikuwa amemsikia Mungu.

103 Kasema, "Musa, ngoja kidogo, jua limewaka sana, una kasoro. Ha—hali yako ya kiakili si sawa, Musa, rudi ulikotoka."

104 Ati ujaribu kumzuia! Usingeweza kumzuia. Mungu alikuwa amemwambia ataiteka, naye akaiteka. Huenda akatenda kiajabu, lakini alijua alichokuwa akifanya, alikuwa na nia ya Mungu, alijua mapenzi ya Mungu. Alijua alichokuwa akifanya, naye akaenda zake. Na mtu yeyote anayeweza kuingia katika hali hiyo, anajua hasa kile Mungu alichomwitia kufanya, jambo fulani litatokea. Naam, bwana. Sijali ni nani, jinsi ulivyo mgonjwa, yote kuhusu hilo, huna budi kuliamini, ndipo unakuwa wa kung'ang'ania. Hakuna kitakachokuzuia. Hiyo ni kweli.

105 Maskini Daudi, akiwa amesimama pale chini siku hiyo, akatazama kule, na kulikuwa na maskini yule Goliathi mkubwa amesimama pale, vidole inchi kumi na nne, na mkuki wa sindano ya mfumaji ulikuwa mkononi mwake, naye huyo hapo Sauli, tangu mabega hata kichwa mrefu kuliko jeshi lote.

106 Naye maskini Goliathi, mwajua, hivyo ndivyo adui afanyavyo, anapokuweka mahali ambapo anataka kuisugulia kidogo, alisema, "Tusiwe na umwagaji damu." Kasema, "Hebu—hebu mmoja wenu ninyi watu atoke apigane nami, na—na kama ataniua taifa la—langu litawatumikia na kama nikimwua, taifa lenu litanitumikia mimi." Mnaona jinsi wanavyotaka kulifanya, maana alifikiri alikuwa nao.

107 Lakini alisema hilo wakati mmoja mbele ya mtu aliyemjua Mungu. Si mtu aliyefunzwa tu kijeshi, hakujua lolote kulihusu, bali alimjua Mungu, maskini Daudi. Biblia ilisema alikuwa mwekundu, maskini jamaa mdogo huko nje, mwenye mabega yaliyoinama, gunia dogo ubavuni mwake *hapa*, na mkoba mdogo wenye chakula cha kondoo ndani yake, alikuja kule kuwatembelea ndugu zake.

108 Akasema, "Mnataka kuniambia kwamba mtamruhusu huyo Mfilisti asiyetahiriwa, asimame hapa, na kuyatukana majeshi ya Mungu, akisema siku za miujiza zimepita?" Loo, jamani. Huyo alikuwa mtu wa aina gani! Mtu mdogo zaidi wa kundi zima, mtoto tu.

109 Lakini nini? Alijua, alisema, "Ninii. . .Siku moja, moja ya. . .simba aliingia na kuchukua kondoo wa baba yangu na kuondoka naye. Nilimfuatilia na kombeo langu, nikamrudisha. Dubu akaingia, nami nikamwua huyo dubu." Akasema, "Naye

Mungu yeye yule," Haleluya! "aliyeniokoa na simba na dubu atamtia Mfilisti huyo asiyetahiriwa mkononi mwangu." Hebu mkomeshe kama ungeweza!

110 Loo, Sauli, wakamleta tu mbele ya Sauli, jemadari, basi Sauli akasema, "Sasa, mwanangu, ninavutiwa na ujasiri wako, lakini unajua, huna elimu nyingi juu ya mapambano, hujui jinsi ya kufanya hivyo. Labda tutakuweka tu kwenye . . . hebu jaribu deraya yangu." Naye akavaa kitu hicho kikubwa mno, maskini Daudi alikuwa na matege alipoivaa. Alikuja kugundua kwamba ninii . . . deraya yake ya kikanisa haikumfaa mtu wa Mungu.

111 Hivyo akasema, "Tupilia mbali kitu hiki, sijui lolote kukihusu. Sijui lolote kuihusu hii hapa, haya yote hapa jinsi ya kusema 'Amina' vizuri tu, huku neno lako na sarufi ikiwa sawa tu." Kasema, "Acha nipitie njia ambayo nimemwaminia Mungu, acha niende na kile ninachoamini." Amina.

112 Nanyi mnajua kilichotokea. Hakika. Aling'ang'ania, hakuna mtetemo hata mmoja damuni mwake, akatoka pale na kuokota mawe matano, Y-e-s-u [Eng. J-e-s-u-s—Mfa.], akashika hilo kombeo kwa vidole vitano, i-m-a-n-i, imani katika Y-e-s-u, na huyu hapa anakuja akimtumainia Mungu kufanya yaliyosalia.

113 Hayo tu ndiyo yakupasayo kufanya, kumwamini Yesu, Kifo Chake, kuzikwa, kufufuka, kuwapo Kwake kila mahali, utu Wake sasa, ahadi Yake, karama Zake, kudhihirishwa Kwake. Hivyo tu ndivyo unavyopaswa kufanya, kuamini, na kukabiliana na aina yoyote ya kizuizi, kiitwe kansa, kupooza, chochote kile, kabiliana naye ardhini.

114 Mungu anayeweza kuinua nafsi yako yenye dhambi kutoka katika maisha ya dhambi anaweza kukuweka huru na maradhi au ugonjwa wowote ulio nao. Huna budi kuwa na imani hiyo, ng'ang'ania, shikilia, usiiachilie, unaona.

115 Lakini huwezi kuihadaa, haitachukua udanganyifu. Unaweza kuwa sawa kudanganya hapa katika . . . Unaenda kule ambako tunakutana na waganga na hao wengine, hao mashetani, usijaribu kuwahadaa, huna budi kuwa na kile unachozungumzia kwenye huduma za kimishenari. Kabisa.

116 Sasa, huku, mko katika kundi la wasomi hapa Marekani, wanachukua mambo ya kiakili. Hiyo ndiyo sababu hii huduma haikwenda vizuri sana hapa, kiakili tu, kiakili. Lakini sikutumwa kwa kundi hilo kwa vyovyote vile, nilitumwa kwa kundi ambalo, kama alivyokuwa Ibrahimu, lile lililoitwa litoke. Naam.

117 Hapo, Samsoni. Sasa, watu wengi walifikiri kwamba Samsoni alikuwa na . . . Nimeona picha yake imechorwa na, ilionekana kama, alikuwa na mabega, ukubwa wa mlango wa ghala. Mbona, hakuna . . . Ati mtu mkubwa hivyo? Lisingekuwa fumbo jinsi mtu kama huyo angeweza kumchukua simba na kumrarua vipande viwili. Lakini alikuwa maskini mduvi

mwenye nywele za mawimbi, jamaa mdogo sana, maskini vishungi saba vikining'inia mgongoni mwake kama mvulana wa mama, maskini dandoadume. Sasa, kuona jamaa kama *huyo* akimwua simba, kuna jambo fulani. . . si ajabu Wafilisti walijiuliza zinakotoka nguvu hizo zilizofichika.

118 Kwa nini? Angewezaje kuwa na uhakika hivyo? Alikuwa Mnadhiri, alikuwa na nadhiri kutoka kwa Mungu. Hmm! Je, unajua kwamba kila mtoto wa Ibrahimu ni Mnadhiri akiwa na nadhiri kutoka kwa Mungu, aliyoapia kwa nafsi Yake?

119 Maskini Samsoni, jamaa mdogo mwenye nywele za mawimbi, maskini. . . maskini vishungi saba vilivyoning'inia mgongoni mwake, simba akaja akinguruma, Samsoni alikuwa mtu mdogo amesimama pale, lakini mnaona, Roho wa Bwana akaja juu yake. Hiyo ilileta tofauti. Mwangalie akisimama nje kondeni, siku hiyo, ambapo Wafilisti elfu moja walimzunguka, alitazama pande zote, asingeweza kuwa na kitu, yeye. . . kupigana nacho, akaangalia chini, akaokota mfupa wa taya ya nyumbu.

120 Vema, mtu yeyote anajua mfupa wa kale wa taya ya nyumbu uliopauka. . . Nazo hizo kofia za Wafilisti zilikuwa na unene wa zaidi ya inchi moja ya shaba, na vazi la kile wanachokiita "deraya," ambalo lilikuwa ni chuma kilichopandana, chini namna *hiyo*, na pamoja na mikuki, na ngao kubwa, wakiwa elfu moja. Lakini Roho wa Bwana akamjia maskini mduvi huyo, akanyoosha mkono kule nyuma na kushika hivyo vishungi saba, alijua bado alikuwa Mnadhiri. Haleluya! Alichukua kile kilichokuwa mkononi mwake, na kuyaponda hayo mafuvu ya kichwa kwa hilo taya kuukuu.

121 Kila mtu anajua ukigonga moja ya mafuvu hayo kwa huo mfupa wa kale wa taya, ungeweza kuruka vipande milioni moja, lakini Mungu alikuwa pale apate kulishikamanisha, naye akawapiga na kuwaua Wafilisti elfu moja. Alikuwa aking'ang'ania. Kwa nini? Hakuogopa, aliweza kuhisi nadhiri hiyo ya Mnadhiri pamoja naye. Haleluya!

122 Mwanamume au mwanamke anayeweza kuhisi Uwepo wa Yesu Kristo, ajue kwamba umezaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu, usiruhusu chochote kikuzuie. Kung'ang'ania, Mungu anaponena na kusema, "Ni wewe, ninakupa imani usiku wa leo. Uponyaji wako ni hakika. Ni Neno Langu," basi unaweza kung'ang'ania. Hakika.

123 Yohana Mbatizaji aling'ang'ania sana kwamba angemwona Masihi. Sasa, Yohana alizaliwa. . . Hatuna mengi kumhusu. Tunajua baba yake, Zakaria, alikuwa kuhani, kutoka katika ukoo wa makuhani. Lakini Yohana kamwe hakufuata nyayo za baba yake, Ujumbe wake ulikuwa mkuu sana, hangeweza kumudu kupitia katika njia ya kikanisa ya siku hiyo, kamwe huwezi.

124 Yohana alijua . . . Wazazi wakongwe, wakiwa wakongwe wakati Yohana alipozaliwa, walijua kwamba, lazima liwe jambo fulani, mvulana huyu, huzuni kwao, walimjua mvulana wao, kamwe wasingeweza kumwona, kwa sababu uzee ungewachukua kabla wakati wake haujafika, bali walijua angekuwa nabii. Bwana alikuwa amenena juu yake, nao walijua hilo. Jinsi hapana shaka liliwaudhi hao mume na mke.

125 Tunaambiwa, kulingana na historia, yapata umri wa miaka tisa, kumi, huyo mvulana, baba na mama yake walikufa naye akabaki peke yake. Badala ya kwenda seminari kufanya jinsi baba yake alivyofanya . . . Kazi yake ilikuwa muhimu sana, Mungu hakuweza kumwacha achanganyikiwe. Kulikuwa na baadhi ya hao jamaa waliosema, "Sasa, Yohana, wewe utamtambulisha Masihi, sivyo?"

"Naam, bwana. Hiyo ni kweli."

"Vema, unajua, Dk. *Nanii*, Askofu Mtakatifu *Nanii* hapa? Je, huoni kwamba yeye ni mtu anayefaa hapo?"

"Loo, nafikiri . . . "

"Loo, la, Rabi, umekosea. Askofu Mtakatifu *Nanii anafaa* tu kabisa."

126 Sasa, ungeweza kupata upuuzi kama huo, kuchanganyikiwa? Yohana hangejichanganyisha, upuuzi kama huo. Mnajua alikoenda? Alienda nyikani, peke yake pamoja na Mungu. Naye Mungu akamwambia huko nje, akakutana naye nyikani, na kusema, "Yohana, utakayemwona Roho akimshukia na kukaa juu Yake, Huyo Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto."

127 Yohana alikuwa na hakika sana kwamba angemtambulisha, akasimama ukingoni, akasema, "Kuna Mtu amesimama miongoni mwenu sasa ambaye hata hamjui." Amina. Alijua alikuwa yuaja wakati huo. Walikuwa wamemtazamia kwa miaka elfu nne, lakini akasema, "Kuna Mtu aliyesimama kati yenu sasa hivi msiyemjua, Huyo Ndiye."

128 Huwezi kusema "*Huyu*, *yule*." Mnaona, ilimbidi kushika mafunzo yake sawasawa, ilimbidi ajue hiyo ishara ya Kimasihi. Ilimbidi ajue huyo Masihi angekuwaje. Mungu angeonyesha kutoka Mbinguni kile Masihi huyo alikuwa. Naye Yohana akasema, "Sikumjua. Lakini Yeye aliyeniambia nyikani, 'Nenda ukabatize kwa maji,' alisema, 'Ambaye Roho atamshukia na kukaa juu Yake, na'" Yohana alisema, "nashuhudia," amina, "ya kwamba Huyo ni Mwana wa Mungu, maana nilimwona Hua akishuka." Hakuna mtu mwingine aliyemwona; hakuna mtu mwingine aliyekuwa akimtafuta. Lakini Yohana alikuwa akimtazamia, naye Yohana akamwona.

129 Sijali ni wangapi wanaoshindwa katika uponyaji wao, wewe amini ya kwamba ni wewe. Wewe ushikilie. Sijali alichofanya

Jones, ama hao wengine, wewe ushikilie na kung'ang'ania Mungu anapokufunulia kwamba Mwanawe amekuweka huru na dhambi na magonjwa. Wewe ushikilie, ng'ang'ania. Naam. Yohana alijua.

130 Aisee, afadhali niache, sitapata kulifikia somo langu. Mnajua nini? Mwanamke huyu alikuwa Myunani, niliyekuwa namzungumzia, naye alikuwa wa taifa lingine, na, lakini alisikia habari za Yesu. Imani huja vipi? Kwa kusikia, kusikia Neno. Ulisema, "Vipi . . . " Vema, alisikia habari Zake, Yeye ni Neno. Kwa hiyo Yeye alikuwa Neno, naye akasikia.

131 Sasa, alikuwa na upinzani mwingi. Lakini sikilizeni hili sasa, imani hupata chanzo ambacho wengine hawaoni. Imani hupata chanzo ambacho wengine hawawezi kukiona. Imani ni dhihaka kwa kila mtu isipokuwa Mungu na mtu aliye nayo. Ni dhihaka kwa kila mtu isipokuwa Mungu na mtu ambaye ana imani, sasa ni—ni—ni dhamana kwao. Ni yakini kwa Mungu, na ni yakini kwa mtu aliye nayo, lakini hao wengine wanafikiri kuwa wana wazimu, sikuzote wamedhania hivyo. Lakini ni yakini kwao.

132 Neno Lake ni Upanga. Waebrania 4:12 inasema kwamba Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili. Sasa, upanga wa imani la- . . . Upanga wa Neno lazima ushikwe kwa mkono wa imani. Hakuna kitu kingine kinachoweza kuutumia huo Upanga ila imani katika Neno.

133 Sasa, baadhi ya watu wanaweza kuchukua Neno na—na kukata vya kutosha kujiunga na kanisa. Huo karibu ndio umbali wangeweza kufika. Wengine wanaweza kukatia ndani, kukata kila ahadi ya Mungu, kukata ahadi ya Roho Mtakatifu, kukata uponyaji wa Kiungu. Inategemea jinsi mkono huo wa imani unaoshika huo Upanga ulivyo na nguvu.

134 Kila ahadi ni yako. Ni mkali vya kutosha kukata kila kitu kilicho karibu nawe, na kukufanya mwana na binti wa Mungu, huru kwa yote. Lakini inategemea ni mkono wa aina gani unaoushikilia huo Upanga, lazima uwe ni mkono wa imani.

135 Huenda maskini mwanamke huyu alikuwa na vizuizi vingi, lakini imani yake haikuwa na chochote. La. Unaweza kuwa na vikwazo vingi. Labda daktari wako anasema haiwezi kutendeka. Lakini kama una imani, haileti tofauti yoyote kile mtu mwingine yeyote asemacho, imani yako haina kizuizi, imani yako inaliona. "Ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana." Ibrahimu aliviita vitu ambavyo havikuwako kana kwamba vilikuwako, kwa sababu Mungu alisema hivyo.

136 Ungeweza kuwazia Ibrahimu, mzee huyo? Sasa, ana umri wa miaka sabini na mitano kabla Mungu hajapata kumwita, Sara alikuwa na sitini na mitano, hiyo ni kama miaka ishirini baada ya kukoma hedhi. Mungu alisema atapata mtoto, naye

atampata, “Kupitia yeye nitaubariki ulimwengu, pamoja naye, mataifa yote. Wakuite baba wa mataifa.”

137 Mnaweza kuwazia mzee, umri wa miaka sabini na mitano, na mwanamke mkongwe, sitini na mitano, wakishuka sasa kwenda kwa daktari, na kusema, “Daktari, tungependa kufanya mipango kwa ajili ya chumba cha hospitalini, kwenda kujifungua mtoto.”

Daktari angesema, “Bwana, una umri gani?”

“Loo, sabini na mitano tu.”

“Mke ana umri gani?”

“Sitini na mitano.”

138 “Loo, loo, hakika, bwana. Nakwambia, toka tu nje polepole.” Angemwita daktari wa magonjwa ya akili, na kushuka, na kusema, “Chunguza akili ya huyo mzee, ana kasoro. Usimwachilie mtu huyo mitaani, yeye ni hatari.”

139 Kwa nini? Kila mtu anayechukua Neno la Mungu hufikiriwa hivyo. Mungu huchukua upumbavu wa kuhubiri ili kujidhihirisha Mwenyewe kwake.

140 Neno Lake, kuamini Neno Lake! Naona siku ishirini na nane za kwanza zikipita. Sasa, unaona, sasa, Ibrahimu alikuwa ameishi na mwanamke huyu tangu alipokuwa msichana mdogo, alikuwa dada yake wa kambo. Aliolewa naye, mwenye umri wa miaka kumi na minane hivi. Na kwa hiyo, akaenda na kusema, “Sara, habari, mpenzi? Tofauti yoyote?”

“Hata kidogo.”

141 “Utukufu kwa Mungu, tutampata huyo mtoto kwa vyovyote vile. Tayarisha vijibuti, na jicho-ndege yote, na pini, na kila kitu. Jitayarishe. Tutampata.”

“Unajuaje utampata?”

“Mungu alisema hivyo.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Mwezi wa pili ukapita, “Unajisikiaje, Sara?”

“Hakuna tofauti.”

“Utukufu kwa Mungu, ni mwujiza mkuu zaidi kwa mwezi mwingine mmoja. Haleluya!”

Mwaka ukapita, “Unajisikiaje, mpenzi?”

“Hakuna tofauti.”

“Utukufu, ni mkuu zaidi kwa mwaka mmoja.”

Ndipo miaka ishirini na mitano ikapita, “Unajisikiaje, Sara?” Mkongwe na mnyonge, “Unajisikiaje?”

“Hakuna tofauti, mpenzi.”

“Utukufu kwa Mungu, ni miaka ishirini na mitano zaidi ya mwujiza.”

142 Nasi tunasema sisi ni Uzao wa Ibrahimu. Uh-huh. Tuna Roho Mtakatifu, "Vema, niliombewa jana usiku, lakini hakika sikupona." Wewe ni kisingizio duni kwa Uzao wa Ibrahimu. "Ibrahimu aliviita vitu visivyokuwepo kana kwamba vilikuwepo." Amina. Haleluya! Kwa maana aliamini yale ambayo Mungu aliahidi, Mungu alikuwa mkubwa vya kutosha kutimiza Neno Lake. Amina. Haya basi. Uzao wa Ibrahimu, hebu nisiingilie hilo.

143 Sasa, mwanamke huyu alikuwa na upinzani mwingi, alikuwa Myunani. Na sasa, yeye alikuwa mfuasi wa dhehebu lingine, nao wangesema, "Sasa, ngoja kidogo, wewe ni Myunani, usishuke kule, kwa sababu mchungaji wetu haufadhili." Loo, samahani. Sawa. Hata hivyo, "Unajua, wewe ni wa *hili*. Usi—usishuke huko chini sasa, kwa sababu . . . "

144 Lakini hilo halikumzuia, alikuwa na imani. Imani ilikuwa imeshikilia. Mbona? Alikuwa na binti aliyehitaji uponyaji, naye alijua kulikuwa na nguvu za uponyaji. Alisikia kuhusu Yeye kuwaponya wengine, "Imani chanzo chake ni kusikia," naye huyu hapa. Akaendelea mbele kwa vyovyote vile, hilo halikumzuia.

145 Labda alikutana na kikundi kingine, wanasema, "Sasa, angalia mpendwa. Sasa, Melinda," Melissa, kitu kama hicho, chochote kile labda, walichomwita. Natumai hakuna mtu hapa mwenye jina hilo. Lakini hata hivyo, ni sawa, ingekuwa ni heshima. "Aisee, sikiliza, Melinda. Unajua nini? Siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama hicho. Usiende huko chini, utaleta fedheha tu."

146 Aling'ang'ania. Imani ilikuwa tayari imetia nanga mle ndani, haijalishi kama mchungaji alikuwa akishirikiana, kama dhehebu lake liliamini au la, kama watu wake waliliamini, kama kuna mtu yeyote aliyeamini mbali na yeye. Imani ni kitu cha mtu binafsi. Naam, bwana. Ni yeye, kama siku za miujiza zilipita kwa hao wengine ama la, haikuwa kwa ajili yake.

147 Kulikuwa na jamaa aliyeniambia si muda mrefu uliopita, akasema, "Sijali ni watu wangapi ungewaponya," au kadhalika namna hiyo. Kasema, "Siamini katika uponyaji."

148 Nikasema, "Hakika. Haukuwa kwa ajili ya wasioamini, ulitumiwa tu waaminio, ni kwa ajili yao tu, waaminio tu." Loo, kutokuamini kwako hakukupeleki popote, kunakuzuia tu, hivyo tu, hakumzuii Mungu; Mungu anaendelea moja kwa moja kulifanya vivyo hivyo.

149 Wakasema, "Huwezi kumpata Roho Mtakatifu, alitolewa tu kwa ajili ya wale mitume kumi na wawili." Hilo halimzuii Mungu, Yeye anaendelea moja kwa moja kulitenda, watu wakimpokea. Huenda wasiweze kuuelezea, lakini wanao vivyo hivyo hata hivyo.

150 Siwezi kuwaambia jinsi ng'ombe mweusi anavyoweza kula majani ya kijani kibichi, kisha anatoa maziwa meupe, lakini yeye hufanya hivyo, kweli kabisa. Kwa hiyo siwezi kulielezea, sijui jinsi inavyofanyika, lakini i—inafanyika kwa vyovyote vile. Sijaribu kulielezea. Kama unaweza kumwelezea Mungu, basi si imani tena. Kila kitu unachopata kutoka kwa Mungu huja kwa imani. Amina. Huwezi kukielezea. Huwezi kumwelezea Mungu, unamwamini Mungu. Amina.

151 Sasa, "Siku za miujiza zimepita." Aling'ang'nia. Dada mwingine mzuri alikutana naye pembeni labda, na kusema, "Unaenda wapi asubuhi hii?"

"Ninaenda kukutana na Yesu wa Nazareti."

"Loo, yeye—yeye si wa dhehebu letu."

"Haileti tofauti yoyote, nina binti aliye na haja, naye ataponywa. Nitampeleka . . . "

152 "Unajua nini? Nakwambia, najua mumeo ni mfanyabiashara hapa mjini, atakuacha. Hakika tu kama vile unavyokwenda, utakuwa na kesi ya talaka." Bado alikuwa aking'ang'ania. Alikuwa anaenda, kwa vyovyote vile. Aling'ang'ania sana.

153 Baadhi yao walisema, "Unajua, Melinda, utakapokuja kanisani tena, utakuwa, ndiye wa kuchekwa kanisani, kwa sababu unashuka kule kujipumbaza tu, kujichanganyisha, kundi hilo la watakatifu wanaojibingirisha. Na haya—haya basi. Unaona, utahesabiwa kama mmoja wao. Kila mtu kanisani atakucheka utakapoenda Jumapili ijayo."

154 Bado alikuwa aking'ang'ania. Hakuna kitakachomzuia. Anaendelea kwa vyovyote vile. Nini? Imani ilikuwa imetia nanga. Aling'ang'ania, hakuna kitu kitakachomzuia, angeendelea kwa vyovyote vile. Naam.

155 Halafu basi, huyu hapa anakuja mmoja wa wazee wa kanisa, na kusema, "Unajua nini? Ukishuka kwenye mkutano huo, ninakwambia kitakachotukia, utafanywa *wa kanisa*. Ni hayo tu. Watakuondoa kanisani. Mara tu utakaposhirikiana na kundi hilo la watu kule chini na ulokole huo, hakika utaondolewa kanisani."

Alikuwa bado anang'ang'ania, alikuwa akienda. Hakuna kitu kitakachomzuia, alikuwa anaenda kufika huko.

156 Naye huyo akaenda zake. Hatimaye akawasili. Sasa, alidhani yote yamekwisha, hakuna lingine. Kwa hiyo alimpomjia Yesu, alisema . . . Aliwasikia hao wengine, katika kumwita, "Mwana wa Daudi," akasema, "Ewe Mwana wa Daudi." Sasa, yeye alikuwa Mmataifa, hakuna "Mwana wa Daudi" kwake, Yeye, huyo. Akasema sasa, "Ewe Mwana wa Daudi, umrehemu binti yangu." Ndipo akakutana na masikitiko baada ya kufika kwa Yesu. Loo, jinsi ilivyo ya kigeni, lakini alikabiliana nayo. Alipata masikitiko.

157 Yesu alimjulisha, kwamba "Sijatumwa kwa jamii yako, nimetumwa tu kwa Wayahudi." Loo, jamani. Hilo lingetoa baadhi ya upepo kutoka kwetu sisi Wapentekoste! Si yeye, alikuwa ameshika kitu fulani. Kasema, "Sijatumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. Sijatumwa kwenu, jamii yenu, watu wenu, sijatumwa hata kidogo."

158 Baada ya yeye kupita vizuizi hivi vyote kufika Kwake, kisha alipofika Kwake, kumsikia akisema kwamba "Sijatumwa kwenu, jamii yenu," hilo litasimamisha imani? La, bwana.

159 Ndipo basi akasema, "Jambo lingine, ninyi si kitu ila kundi la mbwa." Loo, jamani. Hilo—hilo lingetugonga sisi Wapentekoste! Loo, jamani, tungelilipuka kama chura akila risasi. Tungekuwa na . . . Mbona tungekuwa na . . . Ingekuwa mbaya sana. Tuna . . .

160 Lakini yeye hakuwa mmea wa tuta. Haikumbidi kunyunyiziwa kama mmea wa tuta. Hakuwa chotara, kama baadhi ya mazao ya siku hizi. Alikuwa ameshikilia imani. Haleluya! Shida yake ni kwamba siku hizi, tuna mambo mengi sana ya kichotara. Hiyo ni kweli kabisa.

161 Nilisoma makala katika *Reader's Digest*, si muda mrefu uliopita, ambapo watu, wanawake wetu wakila nyama hii chotara, mahindi chotara, na upuuzi huo wote, chembe za mahindi, kwamba wanakua wembamba kwenye nyonga. Na miaka ishirini kuanzia sasa, wasipofanya kitu, sayansi inasema kwamba mwanamke hawezi kujifungua mtoto wake. Inaua. Chochote ambacho ni chotara ni mbaya.

162 Nilishuka huku, nikaona ubao mkubwa sana, ukasema, "Ya Funk" au kitu kama hicho, "Mahindi Chotara, yaliyo bora zaidi." Masuke makubwa mno, mazuri, lakini hayafai kitu. Hayafai kitu, hebu jaribu kuyapanda uone kitakachotokea.

163 Sasa, hiyo inachukua sayansi na kuthibitisha hoja zao wenyewe si sahihi, kuhusu asili ya mwanadamu. Hebu chukua chochote na kukichanganya, kukichanganyia mbegu, wala hakiwezi kujizalisha tena. Hebu chukua fa—farasi jike na kumzalisha na punda dume, naye atazaa nyumbu. Lakini nyumbu huyo hawezi kuzaa tena na kupata nyumbu mwingine, inamwua papo hapo. Hiyo ni kweli.

164 Na chochote ninachofikiri ni kijinga ni nyumbu, chotara, maskini masikio makubwa mno marefu, yaliyowekwa pale. Unajua, huwezi kuwaambia kitu. Tuna dini nyingi kupita kiasi za nyumbu siku hizi, hiyo ndiyo shida ya ulimwengu. Wanaketi hapo na huo uso mrefu wa utakatifu, mwajua, na kusema . . . ningesema . . . kuhubiri uponyaji wa Kiungu, na nguvu za Mungu, wanasema, "Hoo, hoo. Siku za miujiza zimepita. Siamini upuuzi huo wa kale. Kamwe usininii . . . Hoo, hoo." Dini tu ya kale ya nyumbu, ya kijinga. Hivyo tu. Hajui anakotoka, kamwe huwezi kumfundisha chochote. Haijalishi,

atasubiri maishani mwake mwote, apate kukupiga teke kabla hajafa, unajua hilo.

165 Nimejishughulisha na farasi, nikafanya kazi kwenye ranchi, najua ninachozungumzia. Kitu hicho ni maskini baradhuli tu. Lakini basi . . . Hujui alikotoka. Hajui baba yake ni nani, mama yake ni nani, wala chochote kile.

Ndivyo ilivyo kwa baadhi ya hizi dini chotara siku hizi, hawajui baba yao ni nani. Ukisema, "Mbona, wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni Mmethodisti." "Mimi ni Mbaptisti." "Mimi ni Mpresbiteri. Mimi . . . " Loo, hata hujui unakotoka.

166 Lakini loo, jinsi ninavyompenda farasi ukoo safi! Ndugu, anaweza kukwambia . . . Wanaweza kuangalia ukoo wake, nawe unaweza kuona baba yake alikuwa nani, babu yake, nyanya yake, huko nyuma kabisa kwa sababu yeye ni ukoo safi.

167 Nami ninapenda kumwona Mkristo ukoo safi halisi aliyezaliwa kwa Neno la Mungu. Anajua alikotoka, anajua Baba yake ni nani, anajua Mama yake ni nani. Sio madhehebu fulani ya kijamii, ni nguvu za Mungu, Mwana wa Mungu, alikufa kwa nafsi yake, na kuzaliwa upya mara ya pili. Yeye ni kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Yeye ni mpole, unaweza kumwambia jambo fulani, ataitikia kila Neno la Mungu kwa "Amina."

"Je, unaamini *hili*?"

"Amina."

"Siku za miujiza ziko hapa."

"Amina."

"Yesu Kristo yeye yule jana, na hata milele."

"Amina." Najua—najua alikotoka. Naam, bwana. Yeye ni mwana wa Mungu. Naam, kwa kweli.

168 Lakini huyo nyumbu, huyo chotara, alibaniwa *hapa* kisha akahamisha karatasi zake kutoka kanisa moja hadi lingine, hadi lingine. Kwa nini usiliweke Mle wakati mmoja, kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo ambamo halitaondolewa? Amina. Mnajua ninajisikia kubarikiwa sana sasa hivi, mimi mwenyewe. Nena kuhusu . . . Ninajisikia kama ningeweza kupaza sauti. Naam, bwana. Loo, hakika. Yeye . . . Haikukubidi kumnyunyizia tena.

169 Chotara. Loo, mnasema, "Tuna makanisa bora zaidi." Na hiyo ndiyo shida ya Wapentekoste wetu, kupata jambo lile lile. Loo, tunawazia juu ya jengo fulani kubwa mno, zuri, mhudumu fulani wa kiakili anayeweza kusimama, na—na kutoka nje na kuidhinisha kuoga mchanganyiko, na kila kitu kingine, na aina hii nyingine yote ya upuuzi, kuwaacha wanawake wakate nywele zao, wavae kaptura, na kadhalika, na kuziita "ukombozi wa wanawake." Upuuzi. Hiyo ni kweli. Ni dhambi, na aibu.

170 Tunachohitaji leo ni uamsho mzuri wa mtindo wa kale wa Mtakatifu Paulo, na Roho Mtakatifu wa Biblia, na nguvu za Mungu zirudi ndani ya kanisa tena kulitoa. Naam, tunahitaji. Hiyo ni kweli kabisa.

171 [Ndugu ananena kwa lugha na mwingine anafasiri—Mh.] Jina la Bwana libarikiwe. Jinsi tunavyomshukuru Mungu! Mungu asifiwe. Naam, bwana. Amina kwa hilo. Tunaamini jinsi Mungu anavyolituma. Angalieni, nasi tunalikubali, kwa usahihi.

172 Mungu anataka Wakristo halisi waliozaliwa mara ya pili. Anataka wanaume na wanawake ambao kweli wamejitolea kabisa kwa Mungu, wala sio . . . Mnajua, Hollywood hung'aa, na watu ni . . . wanajilinganisha kupita kiasi, tuko karibu mno na Hollywood. I—Injili haing'ai, humeka. Hollywood inang'aa kwa mapambo, na kanisa linang'aa kwa mapambo, lakini Ro—Roho Mtakatifu humeka kwa unyenyekevu.

173 Hapa si muda mrefu uliopita, nilikusudiwa kuzungumza huko Chicago, ndipo mhudumu fulani, kwa sababu ya hizo tofauti, yeye . . . sikuwa mfuasi wa shirika lake, walikuwa wamepiga kura, nao hao watu walitaka nije niwazungumzie, nisingeweza kufanya hivyo kwa vyovyote vile, lakini akasema, "Loo, hapana," kasema, "yeye ni mwenda wazimu wa kawaida." Kasema, "Yeye ni . . . Yote afanyayo ni kuwatukana watu," na kadhalika namna hiyo.

174 Naye akamwalika daktari mashuhuri wa mambo ya kiungu, aje. Alikuja na karatasi za kutosha na mahubiri ya kiakili ambayo hayangefanya chochote. Akapanda pale, kifua mbele, ukosi mkubwa uliopinduliwa, na kuanza kuzungumza, mwajua, huku maneno yake yanayovutia sana, na namna hiyo. Na loo, jamani. Naye akagundua kwamba haikuendana na watoto wa Mungu; waliketi tu pale na kukodoa macho.

175 Basi baada ya muda kidogo akagundua halikolei, kwa hivyo akafunga muhtasari wake wote, kisha akashuka jukwaani huku mabega yake yamenyenyekea namna *hii*.

176 Kulikuwa na mtakatifu mzee ameketi pembeni, akamgusa huyo mwingine, kasema, "Kama angalipanda jinsi alivyoshuka, angeshuka jinsi alivyopanda." Hivyo ndivyo tu ilivyo leo, ndugu. Tunapaswa kushuka, hatuna budi kushuka kwenye Roho Mtakatifu tena, hadi kwenye Biblia, kurudi kwenye Neno halisi la Mungu.

177 Maskini mwanamke huyu, alikuwa na mambo ya kila namna ya kumzuia. Alipofika kwa Yesu, yeye . . . Yeye akamwita mbwa, akasema, "Haifai kukitwaa chakula cha watoto, na kuwatupia mbwa."

Basi angalieni. Kama huyo angekuwa mmoja wetu Wapentekoste, "Vema, sitarudi na kumsikiliza huyo mtakatifu anayejibingirisha tena. Naam, bwana. Watu walisema kweli."

178 Lakini vipi yeye? Sio yeye. Alikuwa ameshika imani. Alikuwa na kitu ambacho alikuwa anaenda kufanikisha, uponyaji wa binti yake. Haidhuru Yeye alisema nini. Angalieni, u—ukweli . . . Na unyenyekevu daima utakubali ukweli ni sahihi.

179 Akasema, "Ni kweli, Bwana. Mimi si wa watu Wako. Mimi si Myahudi, wala mimi si kitu ila mbwa. Hiyo ni kweli kabisa, Bwana. Wala haifai kwako kuchukua mkate wa watoto na kutupatia sisi mbwa. Lakini, Bwana, mbwa hula makombo chini ya meza ya watoto." Alikuwa tu akitafuta makombo. Wakati, hatujaalikwa kwenye makombo, tumealikwa mezani, lakini yeye alikuwa akitafuta makombo.

180 Kumbukeni, yeye alikuwa Mmataifa, hakuwa amewahi kuona mwujiza. Lakini kitu kilikuwa kimetia nanga ndani yake kwamba aliamini mmoja. Hakuhitaji kuona chochote kikifanyika. Hawakuwa . . . Hakuhitaji kumthibitishia kuwa alikuwa Masihi.

181 Yeye alikuwa kama yule kahaba Rahabu. Wapelelezi walipokuja, walimkuta kahaba Rahabu, hawakuninii . . . Yeye hakusema, "Nileteeni Yoshua. Hebu nione jinsi anavyovalia nguo zake, jinsi anavyosimama wima. Je, ana sura nzuri? Je, anachanua nywele zake? Anafanyaje . . . ?" Yeye hakutaka . . . "Nini . . . ? . . . Hebu nimwone akifanya hivyo."

182 Alisema, "Nimesikia. Hiyo inatosha kwangu. Nimesikia." Ndipo akang'ang'ania. Akasema, "Najua tutaangamizwa. Nifanye nini? Nipe kibali. Acha niiokoe nyumba ya baba yangu." Loo, jina lake halipatikani na makosa. Yeye ni mmoja wa nyanya wa nyanya wa Bwana wetu Yesu Kristo, bila shaka, kwa sababu aliamini.

183 Sasa, mwanamke huyu alisema, "Bwana, najua mimi si mwema. Najua taifa letu ni kundi la makafiri, lakini ninajua ya kwamba sisi si kitu ila kundi la mbwa, lakini ninatafuta tu makombo, Bwana. Binti yangu ni mgonjwa huko, nami ninajua unaweza kulitekeleza."

184 Ndipo akaanguka chini na kumwabudu. Loo, jamani. Loo, hilo linaniua tu. Akaanguka chini, akasema, "Kweli, Bwana, mimi si kitu ila mbwa." Angalieni yale maskini huyo mwanamke aliyokuwa amekumbana nayo kufikia hapo.

185 Halafu alipofika hapo, basi akamwita mbwa, na chochote kile, hilo halikuizuia imani yake. Na wakati mwingine tunaweza kuombewa, na kusema, "Huh. Hapana shaka ni bure, sijisikii tofauti hata kidogo." Uzao wa Ibrahimu, Wakristo, wenye kung'ang'ania, tunapaswa kuinamisha vichwa vyetu kwa aibu. Hiyo ni kweli. Naam.

186 Lakini yeye, haidhuru nini, hata alipokuwa Mbele za Yesu Kristo na akakataliwa na Yeye, bado aliendelea kushikilia. Yesu akasema, "Kwa neno hili, ibilisi amemwacha binti yako."

187 Mnaona, alijua jinsi ya kuiendea karama ya Mungu. Hakuja, kasema, "Vema, nitaenda kuona anachofanya. Na kama anaweza kufanya mambo haya, labda ni telepathia ya kiakili, labda ni saikolojia, labda ni udanganyifu fulani, labda ni maigizo." Kamwe asingepata uponyaji wake alioomba. Lakini alikuja kwa njia ifaayo, naye akapokea kile alichoomba. Imani daima hukubali Neno ni sahihi. Aling'ang'ania.

188 Maneno machache tu zaidi sasa kabla hatujafunga, tamshi ninalotaka kutoa hapa. Martha, alipofika kwa Yesu, aling'ang'ania. Kumbukeni, Yesu alikuwa ameondoka nyumbani kwake na kumwacha Lazaro. Ndipo alipougua . . . Na hao watu walikuwa wameacha kanisa lao. Walikuwa wamefanya kila kitu, kisha wakatoka, na kumkaribisha. Walikuwa wamemwona akifanya miujiza, lakini ilipofika wakati wa familia yao, Yeye alikuwa ameondoka.

189 Ndipo wakamtumia wajumbe, Naye akampuuza huyo mjumbe na akaenda mbali zaidi. Nao wakamtuma mjumbe mwingine, Naye akampuuza huyo, hakika, akaendelea mbele.

190 Mbona . . . Alisema tu, "Sifanyi lolote mpaka Baba anionyeshe," Baba alikuwa amemwambia. Ndipo Lazaro alipokufa, alisema, "Nimefurahi kwa ajili yenu sikuwapo, lakini naenda kumwamsha." Kumbukeni, kaburini Yeye alisema, "Nasema hivi kwa ajili yao." Alijua kilichokuwa kinaenda kutukia, maana Baba alikuwa amemwonyesha.

191 Lakini angalieni, Yeye alimjaribu Martha. Huyu hapa anakuja mbio, na, "Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa." Sasa, ilionekana kana kwamba angelimkemea, na kusema, "Kwa nini hukuja? Angalia yale tuliyokufanyia: Tumekulisha, tumekuburudisha, tuliliacha kanisa letu, tuliwaacha marafiki zetu wote kukufuata Wewe, na kila kitu. Tulitoka katika kila kitu tulichokuwa ndani tukufuate Wewe. Halafu wakati ndugu yetu alipokuwa mgonjwa, Wewe . . . "

192 Ilionekana kana kwamba alikuwa na haki ya kufanya hivyo. Lakini wakati mwingine . . . Unasema, "Tuna haki," lakini unapoteza haki zako. Mwana-kondoo hatakuwa na kitu ila sufu, hiyo ndiyo tu anayoweza kutoa, bali hana budi kuipoteza hiyo.

193 Nilikuwa nikiwaambia wanawake, fulani hapa si muda mrefu uliopita, wajionee aibu, wamevaa hizi ninii ndogo, na hizi ninii ndogo, wanaonekana kama soseji isiyo na ngozi wakivaa hizo nguo namna hiyo, jinsi itakavyowalazimu kuwajibika siku ya hukumu kwa kufanya uzinzi. Unaweza kuwa safi kama yungiyungi kwa mumeo au kwa mpenzi wako wa kiume, lakini kumbuka, Yesu alisema, "Kila mtu atamzamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye." Basi huyo mwenye dhambi atakapowajibika kwa kufanya uzinzi, ni nani aliyefanya hivyo?

Wewe. Enyi dada zangu wa Kipentekoste, rudini, rudini kwenye mtindo wa kale.

194 Huyo mama alisema, "Mbona, hata hawatengenezi mavazi mengine ila hayo." Lakini wangali wanatengeneza cherahani na kuuza vitambaa. Hakuna udhuru. Mnaona? Hiyo ni kweli. Ni kweli kabisa. Hiyo ni kweli. Mimi ni . . . Naamini hilo. Kwa hivyo hakuna udhuru. Hata afadhali tulikunje, na kuirudia Injili halisi, na kulirudia Neno la Mungu tena, na kuwa sawa. Hiyo ni kweli. Martha alikuwa na haki.

Akasema, "Vema, ni haki yangu ya Kimarekani kama ninataka kufanya hivyo.

Nikasema, "Naam, lakini ulisema wewe ni Mkristo."

Alisema, "Naam."

Nikasema, "Basi wewe ni mwana-kondoo, na mwana-kondoo hupoteza haki zake."

195 Kama Mkristo Mmarekani, raia wa Marekani, ninayo haki ya kunywa pombe, kuvuta sigara, kufanya lolote nitakalo, kununua pombe, lakini naipoteza hiyo. Mimi si wa . . . Ninaishi katika taifa hili, lakini mimi ni msafiri, Makao yangu yako juu. Kila Mkristo mwingine aliyezaliwa kutoka juu, anaishi kutoka juu.

196 Mke wangu, aliyeketi pale nje, aliniambia . . . Tulikwenda kwenye supamaketi, ni jambo la ajabu nyumbani, tulimwona mwanamke mmoja alikuwa amevaa gauni. Wengine wote walikuwa . . . Nao wanaimba katika kwaya na kila kitu. Akasema, "Billy, hiyo ni nini?"

Nikasema, "Mpenzi, ni roho ya Marekani."

Akasema, "Hivi sisi si Wamarekani?"

197 Nikasema, "La, tunaishi hapa, hapa ni mahali petu pa kimwili, lakini tumetoka juu. Watu wetu wanatenda kama Huko juu, Roho kutoka Huko juu aliwashukia. Na kama nikienda kwenye nchi nyingine, wao husema, 'Huyo ni Yankii, anatoka Marekani.' Ukienda Ujerumani, una roho ya Kijerumani; Uswisi, roho ya Kiswisi. Popote ulipo, una roho ya taifa hilo."

198 Kuna roho miongoni mwa watu. Loo, rehema. Nenda kwenye jambo sahihi. Kuna . . . Kwa nini . . . Ikiwa unaweza kuwa na cha bandia, mbona usichukue kilicho halisi? Kwa nini tupoteze kilicho halisi kwa ajili ya cha uongo, wakati anga zote zimejaa baraka halisi za Kipentekoste? Amina. Kwa nini tuchukue kibadala cha kitu chochote? Amina. Amini kwa moyo wako wote. Usiwe na shaka hata kidogo, lakini uamini kwamba Neno la Mungu ni sahihi. Naam, bwana.

199 Sasa, Martha alimwendea, akasema, "Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa." Loo, jamani. Huko ni kung'ang'ania, kuvunja kila kizuizi. "Kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa."

Akasema, "Mimi ndimi u-. . . Ndugu yako atafufuka tena."

Akasema, "Naam, Bwana, alikuwa mvulana mwema, atakuja katika ufufuo wa kiama."

200 Yeye akasema, "Mimi ndimi Ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Na kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Je, unaamini hili?"

Akasema, "Naam, Bwana. Ninaamini ya kwamba Wewe ndiwe Mwana wa Mungu, aliyekuwa aje ulimwenguni."

201 Haijalishi alikuwa amesikitishwa jinsi gani na matendo mengine, wakati ulikuwa umewadia ambapo alishika imani. Mnajua ni wapi ninaamini aliipata? Aliposoma Biblia, na kuona ambapo yule mwanamke Mshunami . . .

202 Siku hiyo, mwakilishi wa Mungu . . . Mungu hakosi mwakilishi duniani, sikuzote, kila wakati. Na mwakilishi Wake wakati huo alikuwa nabii, Eliya. Naye alikuwa mkongwe, huyu mwanamke Mshunami, hakuwa na watoto. Ndipo Eliya akamwombea, na kumbariki, na kutabiri, na kumwambia atapata mtoto. Naye akampata. Karibu . . . Akafikia umri wa miaka kumi au kumi na miwili hivi, huyo mtoto hapana shaka alipatwa na ugonjwa unaotakana na jua kali, akalia, "Kichwa changu, kichwa changu," karibu katikati ya mchana. Baba aliagiza mtumishi amwingize ndani, akamweka kwenye paja la mama, kisha huyo mtoto akafa. Ni mahali pazuri jinsi gani pa kumpeleka mtoto mchanga, na kumlaza juu ya kitanda cha nabii, ambapo nabii alikuwa akilala.

203 Na kisha akasema, "Tandika nyumbu, nenda moja kwa moja, na usiongee na mtu yeyote, bali endelea."

204 Ndipo nabii alipokuja . . . Mungu huwa hawaambii manabii Wake kila kitu, ni kile tu anachotaka wajue. Naye akasema, "Huyu hapa yule Mshunami anakuja." Akamwambia Gehazi, akasema, "Ana huzuni moyoni mwake, lakini Mungu amenificha." Akasema, "Hujambo? Mumeo hajambo? Mtoto hajambo?"

205 Angalieni hilo, napenda hilo, akasema, "Hatujambo," huku mtoto wake amekufa. Lakini alikuwa mbele ya mtumishi wa Mungu, alijua kama Mungu angeweza kumwambia mtumishi huyo angempata huyo mtoto, angeweza kusema kwa nini alimchukua huyo mtoto. Kwa hiyo akasimama pale kisha akaanguka chini mbele yake, akaanza kufunua.

206 Sasa, hapo ndipo ninapofikiri Paulo alipata kuwekea leso, mnaona. Akasema, akamwambia Gehazi, "Chukua fimbo yangu, jifunge viuno vyako, na kama mtu yeyote akiongea na wewe, usimjibu, endelea tu, weka fimbo hii juu ya huyo mtoto mchanga." Mnaona, alijua chochote alichokuwa amegusa kilibarikiwa, kama angaliweza tu kumfanya huyo mwanamke kuamini hivyo.

207 Lakini imani ya huyo mwanamke haikuwa kwenye hiyo fimbo, ilikuwa katika nabii. Akamshika. Akasema, "Kama Bwana Mungu aishivyo na nafsi yako haifi kamwe, sitakuacha." Basi Gehazi, namaanisha, Eliya akaambatana naye. Naye akaenda kule, na kuulaza mwili wake juu ya mtoto huyo aliyekufa, akaenda huku na huko chumbani, akaweka uso wake juu ya huyo mtoto mchanga, naye mtoto akapiga chafya mara saba na kufufuka. Na kitu gani? Kwa sababu yule mwanamke Mshunami, "Usisimame, usiwe na mambo yoyote ya kijamii, nenda kwenye Neno."

208 Naye alijua, Martha alijua kama—kama Eliya . . . kama Mungu alikuwa ndani ya Eliya kuleta, kutia nanga imani hiyo, ni zaidi sana vipi alivyokuwa ndani ya Kristo, Mwana wa Mungu? Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu alikuwa aking'ang'ania sana usoni pa Yesu. Vivyo hivyo huyo mwanamke Mshunami usoni pa—pa Eliya.

209 Kuna mwanamke huku chini pwani, nilikuwa nikisumulia habari zake. Alikuja nyumbani, nami nilikuwa . . . nikaingia. Naye huyo mwanamke anatoka nje hapa, mahali fulani. Yeye . . . Baadhi ya watu waliopo hapa wanamjua huyo mwanamke, mdhamini, mmoja wao, ameketi hapa sasa, ambaye alisaidia kumtoa nje. Alikuwa na uvimbe wa pauni hamsini, umetokeza nje *hivi.* Nami nilikuwa nimeingia kanisani, nisingeweza kuwaombea wagonjwa usiku huo, nilikuwa tu nimeingia. Nilikuwa nikitaka kutoka.

210 Na—na kwa hivyo, mwanamke huyo akang'ang'ania sana, alikuwa amefika mbali sana, aliwafanya mashemasi na wadhamini wambebe hadi kwenye mlango mdogo ambamo nilitokea. Basi nilipotoka mle, aliunyosha mkono wake na kunishika mguuni, naye akasema, "Ndugu Branham, ninaamini ya kwamba kama utamwomba Mungu, Mungu ataniponya."

Nami nikasimama tu, na kumwekea mkono wangu, kisha nikasema, "Dada, Mungu wa Mbinguni na aiheshimu imani yako."

211 Alikuwa mkubwa *hivi.* Yeye . . . Wasingeweza . . . Ilibidi wambebe, na kwa hiyo wakamweka pale kwenye mlango mdogo wa nyuma wa kanisa. Basi yapata miezi mitatu baada ya hayo, alipitia pale akipaza sauti na kupiga mayowe, akiwa wazi tu kama mimi.

212 Na yapata juma moja ama mawili yaliyopita, huku chini kwenye Jumba la Ng'ombe, huko Los Angeles, kwenye Lango la Kusini, nilikuwa nikisema jambo moja au lingine kuhusu hilo, huko usiku mmoja, naye akaruka kutoka pale, akasema, "Mimi hapa bado." Ninii tu kabisa . . . Kwa nini? Aling'ang'ania, alikuwa amesafiri, alikuwa ametumia riziki yake, alikuwa amekuja juu ya kitu cha kila namna, kwenye trela dogo kuukuu, akijaribu kufika kule, nao iliwabidi kumpakia chakula, na

jinsi ilivyombidi mumewe kufanya. Lakini yeye aling'ang'ania, alikuwa anaenda kudumu Nao. Hakika. Imani yake ilikuwa imeshika Neno, naye angedumu Nalo.

213 Mikaya, wakati kulikuwa na manabii mia nne waliovalia vizuri wamesimama pale wakimwambia Ahabu na wao, "Kwea; Bwana yu pamoja nawe." Mikaya alisema, "Kwea, ukitaka, lakini Bwana aliniambia kwamba . . . nami niliona Israeli wametawanyika kama kondoo mlimani." Kwa nini? Wakati manabii mia nne wakitabiri kinyume na vile alivyokuwa, angewezaje kuwa na uhakika hivyo? Kwa sababu ono lake lililingana na Neno la Mungu, hiyo ndiyo sababu, yeye alijua hilo. Loo, laiti ningalikuwa na yapata saa moja sasa kuhubiri papo hapo.

214 Ikiwa ono lako halilingani na Neno, lisahau ono lako. Unapojua ono lako limenyooka katika Neno . . . Yule nabii mkuu alikuwa amemwambia Ahabu, akamlaani, na kumwambia kwamba mbwa wangeilamba damu yake kwa sababu ya Nabothi mwenye haki, mambo ambayo alikuwa amefanya.

215 Naye Mungu angewezaje, haidhuru manabii hawa walitabiri kiasi gani, na kusema . . . Mbona, walikuwa na sababu sasa, walisema, "Angalia hapa, Ramoth-gileadi, Yoshua alitupa hiyo, hiyo ni yetu. Hayo mahindi yanayolimwa kule, yanapaswa kuwa yakiwalisha Waisraeli, si adui yetu. Hakika, hiyo ni kweli." Mnaona, kiakili walidhani ilikuwa ni sawa.

216 Hapo ndipo unapofikia kiakili, ukijaribu kuweka kitu, na wakati mwingine imani ni kinyume sana nalo. Daktari anasema, "Angalia hapa, huwezi kuishi, Jamani, kansa hii imekuzunguka." Lakini hebu imani itie nanga hapo wakati mmoja, nawe uangalie kinachotukia.

217 Mikaya alisimama pale miongoni mwao. Ninaweza kuwasikia wakikutana. Mnajua, wangemfukuza kwenye shirika la wahudumu. Kwa hiyo wa—walisema, "Mikaya, kama utatabiri jambo lile lile halmashauri yote inalotabiri, unajua, wanaweza kukurudisha tena."

Akasema, "Mimi? Nitasema tu kile ambacho Mungu ataweka kinywani mwangu, kusema."

218 Loo, ndugu, tunachohitaji ni Mikaya wengine zaidi, wana wa Imla, mnajua. Na hiyo . . . Huyu hapa amesimama na hilo ninii kuu, lenye nguvu . . . Akasema, "Kwea," naye akatabiri kinyume, kwa sababu alikuwa . . . huku watu mia nne wamesimama, mmoja wao hata akampiga kofi mdomoni.

Kasema, "Mrudishe mtu huyu, na umweke katika nyua za ndani, gerezani, na kumfunga kwenye mikatale. Nami nitakaporudi, nitamshughulikia."

Akasema, "Ukirudi kamwe, Mungu hakusema nami." Kwa nini? Aling'ang'ania, alijua mahali alipokuwa amesimama.

219 Yule kipofu aliyezaliwa kipofu, macho yake yakaponywa, asingeweza kubishana nao kuhusu theolojia. Wakasema, "Tunajua mtu huyu ni ibilisi, hakubaliani na shirika letu."

220 Akasema, "Ni jambo geni kwangu. Ninyi ndio viongozi wa nchi, na hapa Mtu aliyafungua macho yangu, halikuwahi kufanyika katika ulimwengu wote tulivyopata kujua, halafu ninyi, viongozi wa dini, na ninyi si . . . hamjui alikotoka, hilo ni jambo la kushangaza."

221 Alikuwa na theolojia nzuri sana ya kubishania, sivyo? Hakika alikuwa nayo. Jambo moja alijua, akasema, "Kama Yeye ni mwenye dhambi au la, sijui. Lakini ambapo wakati mmoja nilikuwa kipofu, sasa ninaweza kuona." Amina. Hilo ni jambo moja alilojua kwa hakika. Aliling'ang'ania.

222 Vivyo hivyo Nathanaeli aling'ang'ania kumtambua Yeye kuwa ndiye Kristo, alipoona jambo hilo la ajabu likitukia, aliposema, "Nilikuona ulipokuwa chini ya mtini."

Akasema, "Wewe ni Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli."

223 Maskini mwanamke huyo aling'ang'ania, kisimani, wakati alipomwambia alikuwa na waume watano. Alipofanya hivyo mbele ya kundi la elimu la Kiyahudi, walisema, "Yeye ni Beelzebuli."

Lakini maskni mwanamke huyu alisema, "Naona kuwa Wewe ni nabii. Tunajua ajapo Masihi, atatuambia mambo haya."

Akasema, "Mimi Ndiye."

Sasa, ati umzuie! Huyo akaingia mjini, akasema, "Njoni mwone Mtu aliyeniambia yale nimefanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi hasa."

224 Ungewezaje kumzuia Simoni Petro asihubiri Injili, hata kama hangeweza kuandika jina lake mwenyewe, Yesu aliposema, "Jina lako ni Simoni nawe ni mwana wa Yona"? Alijua huyo alikuwa ni Masihi. Hakuna njia ya kumzuia.

225 Hapa, si muda mrefu uliopita, huko Meksiko (Nami ninafunga.), tulikuwa na mkutano kule, nami nilikuwa na jambo kuu. Ni nchi kubwa ya Kikatoliki. Nanyi nyote, karibu nyote, ninyi wahudumu mnamjua Jemadari Valdena, ndiye—ndiye aliyeniingiza ndani, serikali. Askofu wa kanisa Katoliki akapanda kule, akamwambia rais, kasema, "Vema, unamleta m—mtu asiye Mkatoliki humu ndani."

Akasema, "Vema," kasema, "Jemadari Valdena anasema, ni mtu anayeheshimika."

Kasema, "Loo." Kasema, "Vema, hakuna kitu kama hicho hapa." Kasema, "Wewe . . . Hatuwezi kufanya hivyo."

Akasema—akasema, "Wananiambia kwamba maelfu ya watu hujitokeza kwenye mikutano yake," rais akasema.

Akasema, "Naam, hakuna wanaotoka kwenda kule ila wajinga na wasio na elimu."

Akasema, "Mmekuwa nao kwa muda wa miaka mia tano. Kwa nini ni wajinga na wasio na elimu?" Nadhani hilo lingeyang'oa mabawa yake. Mnaona?

226 Tuliposhuka kule, tulikuwa na siku tatu tu usiku za kukaa. Usiku wa pili huko, sitausahau kamwe. Mzee wa Kimeksiko alipitia jukwaani, maskini mzee mmoja. Nyote mnamfahamu Ndugu Espinoza? Karibu ninyi nyote mnamfahamu, nafikiri yeye ni wa Assemblies of God, alikuwa mkalimani wangu, amesimama kando yangu. Ilibidi *Sauti* ya Wafanyabiashara iandike makala hii. Huwezi kuchapisha chochote gazetini isipokuwa kinaweza kuthibitishwa, mnaona, hivyo basi hapa . . . isipokuwa unatokeza shingo yako kwa kitu kilicho taabuni.

227 Kwa hiyo maskini huyu mzee wa Kimeksiko akaja, alikuwa kipofu. Asingeweza kuona alipokuwa anaenda, mwajua. Naye akanikaribia, alikuwa miguu mitupu, miguu yake mizee inaparuza, na miguu ya suruali yake imechanika, juu namna *hiyo*, koti kuukuu lililochakaa, hana shati, kofia kuukuu mikononi mwake iliyoshonwa kwa kamba, amejaa mavumbi kote.

228 Nami nikaangalia, na macho yake meupe, macho yenye watoto wa macho, naye alikuwa akipitia pale, naye akaingiza mkono mfukoni mwake, akatoa shanga ndogo, kisha akaanza na "Salamu, Maria," mwajua. Ndipo basi nikamwambia, "Zirudishe."

229 Ndipo Ndugu Espinoza akamsimamisha, akaziweka mfukoni mwake, naye, akigugumiza jambo fulani katika Kihispania, sikuweza kuelewa, sijui Kihispania.

230 Kwa hivyo akaanza kumunya-munya jambo fulani, nami nikawazia, "Maskini jamaa mkongwe." Nami huyu hapa nikiwa nimevaa jozi nzuri ya viatu, suti nzuri. Mzee huyo labda aliishi wala hakuwahi kuwa na kitu ila lundo la saladi yenye amiba ya kupikia chapati. Na—na kwa vyovyote vile, kufikia yapata . . .

231 Uchumi wao ni duni sana, ni mbaya sana. Na labda Pancho anapata takriban . . . yeye ni mwashi wa matofali, anapata takriban peso kumi na tano kwa siku, lakini inambidi kufanya kazi kama siku kumi, ajinunulie jozi ya viatu. Vipi kuhusu maskini Pedro, aliye na watoto kumi, akipata takriban peso tatu kwa siku? Atafanya nini, kuwalisha? Martina anaweza kupata moja usiku wa leo, na Pancho anaweza kupata moja, lakini mtu fulani hana budi kujinyima moja, kwa sababu hawana budi kuweka akiba ya kutosha kununua mshumaa wa grisi kuuwashia kwenye madhabahu ya dhahabu ya dola milioni moja.

232 Sio sawa! Nami niliwaambia haikuwa sawa. Nilisema, "Sio sawa. Hupaswi kulipia chochote, Kristo alikufa apate kukuweka huru." Madhabahu ya dhahabu ya dola milioni moja pamoja na

mshumaa juu yake, na kuwaua watu kwa njaa, pamoja na kuhani fulani wa kuibariki. Mshumaa una uhusiano gani nalo? Kristo alikufa, Damu Yake inatuokoa kutoka kwa dhambi na makosa, ni zawadi ya bure ya Mungu. Hufanyi hata jambo moja kwake, ili kustahili. Ni neema ya Mungu.

233 Naye akaja pale, nami nikamshika mikononi mwangu, ndipo nikawazia, "Nitaona kama viatu vyangu vitamtosha." Ningevitoa kisiri, kulikuwa na mhimili mkubwa wa mkono wa ngazi pale, nimpe koti langu, lakini mabega yake makubwa zaidi, na miguu yake mikubwa zaidi.

234 Nami nikawazia, "Maskini jamaa mkongwe, pengine kamwe hajala mlo mzuri maishani mwake." Nami nikawazia, "Na hapo, maumbile . . . Angalia kilichompata, yeye ni kipofu, maskini jamaa mkongwe. Kama baba yangu angaliishi, angekuwa na umri kama huo."

235 Inakubidi kuwahurumia watu, kama huwezi, kamwe huwezi kumsaidia mtu yeyote. Hiyo ni . . . Wewe . . . Hiyo . . . Huna budi kuwahurumia; unapaswa kujichukulia hilo juu yako mwenyewe. Nami nikamkumbatia tu kwa mikono yangu, kisha nikasema, "Baba wa Mbinguni, umrehemu maskini mzee huyu." Nikasema . . . Nikatazama kule nje, nami nikamwona amesimama, akinitazama, mbele yangu huko nje, akiwa na macho yake. Nilijua kama akipata kuyafungua macho yake, yote yamekwisha.

236 Nilingoja dakika chache tu, akapaza sauti, "Gloria a Dios!" Ni "Utukufu kwa Mungu," mwajua. Hapo angeweza kuona vizuri kadiri nilivyoweza, akitembea huku na huko jukwaani.

237 Kesho yake usiku, kulikuwa na . . . Jukwaa lilikuwa na urefu kama huu, limelundikwa tu juu *hivi* kwa shela kuu kuu na kadhalika. Nanyi mnazungumza juu ya kuja na kuketi nusu saa, au saa moja au mbili kanisani? Walikuja saa mbili asubuhi hiyo, sio kuketi chini, kusimama, wakiegemeana, wakiegemeana kama kondoo kwenye jua hilo kali. Wala nisingekuwa huko hadi saa tatu ama saa tatu na nusu usiku huo. Walikaa siku nzima, hakuna kitu, kusimama tu kule wakingojea nije.

238 Usiku huo, mvua ikinyesha, walikuwa wengi sana, loo, jamani, huo uwanja mkubwa, huo uwanja huko nje, wala nisingeweza kuingia. Wakanizungusha upande wa pili, wakanifunga kamba, na kunishusha jukwaani kutoka juu ya uwanja huo, mvua ikinyesha. Kuna yeyote wenu anayemjua Ndugu Jack Moore? Nadhani wengi wenu mnamfahamu. Naye alikuwa pamoja nami, na Ndugu Espinoza, na huko chini katika Jiji la Meksiko.

239 Nami nikatoka, nikaanza kuhubiri, nami nilikuwa nikihubiri *Imani, Kuwa Na Hakika Ya Mambo Yatarajiwayo, Bayana Ya Mambo Yasiyoonekana* naye Ndugu Espinoza akitoa tafsiri. Basi nilipokuwa nikihubiri, Billy akaja, mwanangu,

na kunishika kwenye koti. Kasema, "Baba, itabidi tu ufanye jambo."

Nikasema, "Kwani kuna nini?"

Kasema, "Maskini mwanamke mdogo amesimama pale." Kasema, "Nina mabawabu mia moja na hamsini ama zaidi, wamesimama huko nje." Kisha kasema, "Mañana . . . "

240 Nilimwita *Mañana*, maana yake "kesho." Huyo ndiye mtu mwenda pole kuliko wote ambaye nimewahi kuona maishani mwangu. Alipaswa kunichukua saa moja, naye angenichukua karibu saa tatu. Kwa hiyo basi, na daima nilimwita "Mañana." Naye angesambaza kadi za maombi, naye alikuwa amekwisha kusambaza kadi zote za maombi.

241 Basi mwanamke mdogo wa Kimeksiko ambaye alikuwa amemleta mtoto wake, Mkatoliki sasa, apate kuombewa majuzi usiku, nami nikazungumza juu ya Biblia, jinsi Yesu alivyokuwa, alikuwa ameangalia upambanuzi huo ukienda huko nje na kuwachagua watu hao kwenye kusanyiko hilo na kuwaona wakiinuka kutoka kwenye hivyo vitanda vya wagonjwa, kwa urahisi, wakiamini tu, na kuwaona wakiinuka namna hiyo.

242 Alikuwa na maskini mtoto mdogo, mgonjwa pale, mwenye nimonia, akijaribu kumnyamazisha. Hakupata kadi ya maombi ama chochote kile, naye akafa kesho yake asubuhi, yapata saa tatu ofisini mwa daktari. Na hapa akamchukua mtoto huyo, badala ya kumpeleka kwenye—kwenye chumba cha kuhifadhia maiti, alimleta pale, na kusimama kwenye mvua hiyo, mchana kutwa, akiwa na mtoto huyo aliyekufa. Wala Mañana kamwe hakumpa kadi. Hakuwa na kadi, wala hangekuwa kwenye mstari wa maombi, lakini alidhamiria kufika huko kwa vyovyote vile.

243 Nao wange-. . . alikuwa na mabawabu mia moja na hamsini, ama mia mbili ambao hawangeweza kumzuia maskini mwanamke huyo. Angekimbilia katikati ya miguu yao, aruke juu ya mabega yao, apande juu ya mabega yao, na kuanza kuruka, mmoja . . . huku ana mtoto mchanga aliyekufa mikononi mwake, mwanamke mdogo sana.

244 Ndipo Billy akanijia, akasema, "Baba, itakubidi tu uende huko na kulishughulikia hilo," kasema, "kwa sababu hatuwezi kumfanyia chochote. Anasumbua sehemu hiyo yote ya mahali hapo, huko."

245 Ndipo nikasema, Ndugu Jack Moore, nikasema, "Ndugu Jack, shuka uende, ukamwombee, hanijui, wala hatajua ila kwamba ni mimi. Hawezi kuzungumza Kiingereza, basi nenda tu umwambie, nenda ukamwombee huyo mtoto."

Akasema, "Vema, Ndugu Branham."

246 Akaanza kwenda, nikasema, "Ndugu Espinoza," Ndugu Espinoza anaweza kuwa hapa. Je, uko hapa, Ndugu Espinoza? Ninii . . . Wewe . . . Ni wangapi wanaomjua Ndugu Espinoza?

Mfasi-. . . wa Kimeksiko. Loo, hakika, nilijua mlimfahamu. Kwa hiyo—kwa hiyo alikuwa amesimama pale, nami nikasema, "Ndugu Espinoza, endelea, sema kama nilivyokuwa nikisema." Nikasema, "Kama nilivyokuwa nikisema sasa, kama vile Bwana Yesu, kwa imani Yeye huitumikisha ninii Yake. . . "

247 Nikaangalia, amesimama hapa mbele yangu, na kulikuwako na mtoto mdogo wa Kimeksiko asiye na meno, akicheka tu, akiniangalia. Nikawazia, "Huyo lazima ni mtoto huyo." Nikasema, "Usiseme kitu, Ndugu Espinoza, ngoja kidogo." Ndugu Jack alikuwa akitoka jukwaani yapata wakati huo, nikasema, "Ngoja kidogo, Ndugu Jack." Nikaenda pale, nikasema, "Billy, ufungue huu mstari ukamlete."

248 Walikuwa wakimshikilia kwa sababu haikuwa halali, hao watu wengine walikuwa na kadi za maombi, nao wangekuja pale na kuchukua hizo kadi. Na kwa hivyo wanapaswa kumtendea kila mtu haki, au ukimruhusu mmoja kuja bila kadi, basi u—una ghasia, hakika kabisa, katika kitu kama hicho. Kwa hiyo, basi i—ilibidi asubiri.

Kwa hiyo nikasema, "Ufungueni mumlete."

Akasema, "Baba, hana kadi ya maombi."

Nikasema, "Mlete huku."

Kasema, "Kuna nini?"

Nikasema, "Nimeona kitu hivi punde."

Kwa hiyo wakamleta. Naye huyu hapa akaja pale, akapiga magoti sakafuni, na kusema, "Padre."

249 Nikasema, "La, la, la, la. Simama." Maskini mwanamke mrembo, alionekana yuko kwenye miaka yake ya ishirini, na maskini msichana wa Kimeksiko, na maskini nywele zake zinaning'inia chini, juu ya mabega yake namna *hiyo*, na macho yake makubwa mno, huku machozi yanatiririka mashavuni mwake, akasema, "Padre," huko akisema kitu. Nami nikasema. . .

Ndugu Espinoza akasema, "Ninakuletea, Padre, mtoto wangu, amekufa."

Na—nami nikasema, "Alikufa tangu lini?"

Kasema, "Saa tatu asubuhi ya leo, kwenye ofisi ya daktari."

"Alikuwa na shida gani?"

"Nimonia."

250 Kwa hiyo Ndugu Espinoza. . . Nikaweka mkono wangu juu ya blanketi hilo lililolowa maji, limelowa maji kabisa, huku mvua inanyesha. Nami nikaweka mkono wangu juu ya blanketi hilo dogo lililolowa maji nikasema, "Baba wa Mbinguni, sijui kung'ang'ania kwa maskini mwanamke huyu, lakini dakika chache zilizopita nilipoangalia huko kwenye kusanyiko, nilimwona mtoto mchanga akinitazama akitabasamu. . . "

Alikuwa amemfunika kwa blanketi, huku amemshikilia *hivi*. Nikasema, "Ikiwa huyo alikuwa huyu mtoto, na kwa sababu ya maskini mwanamke huyu kung'ang'ania hivyo kwamba—kwamba Wewe utamponya mtoto . . . "

Yapata wakati huo akafanya "Waah," na kuanza kurusha mateke kwa miguu yake *hivyo*. Alikuwa yu hai.

251 Nikasema, "Ndugu Espinoza, usiweke hilo . . . usininii . . . chukua . . . Weka mkimbiaji amfuatilie mwanamke huyo, washuke kwenda kwenye ofisi ya daktari na kumwacha asaini taarifa."

252 Naye akampata huyo daktari, naye daktari akasaini taarifa, "Nilimtangaza huyu mtoto, pumzi yote imekwisha, asubuhi ya leo, saa tatu."

253 Mtoto huyo mchanga alikuwa baridi na amekauka, na amekufa tangu saa tatu asubuhi hiyo, kisha akafufuka, kwa sababu mwanamke mdogo aling'ang'ania. Alikuwa ameona jambo fulani likitendeka, naye hangechukua "La" kwa ajili yake. Hilo linaonyesha ya kwamba Mungu yeye yule aliyekuwa akimvuvia maskini mwanamke huyu Myunani angeweza kumvuvia mwanamke Mhispania. Naye anaweza kulisukuma jambo lile lile, usiku wa leo, kama mtaamini. Mnaamini? Loo, iweni wenye kung'ang'ania.

254 Bwana Yesu, ninaamini kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu. Uliteseka chini ya Pontio Pilato, ulisulubiwa, ukafa, ukazikwa, ukafufuka siku ya tatu, na u hai hata milele. Uliahidi, "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu," kosmosi, utaratibu wa dunia, "hautaniona tena; lakini ninyi mtaniona. Kwa kuwa Mimi," kiwakilishi nafsi, "nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele."

255 "Ninakuamini, Bwana, ninang'ang'ania usiku wa leo. Imani imeshikilia kwa namna fulani. Ninaamini ya kwamba utaniponya. Ninaamini ya kwamba utaniokoa. Ninaamini ya kwamba utanipa shauku ya moyo wangu, nami ninakushikilia Wewe."

256 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda mfupi sasa. Kwa njia yako mwenyewe, omba kimyakimya kwa muda mfupi tu sasa, ukiomba, "Bwana Yesu, unirehemu."

257 Sasa, Bwana, kwaya hii, ninii, uh, kanisa hili, kundi hili la watu, linangoja kwa saburi. Nimeongea kirefu. Wanaomba, Bwana. Nimewaambia ya kwamba Wewe hujafa, kwamba umefufuka katika wafu. Niliwapa kila ahadi, niliwaambia, jana usiku, ahadi ambayo umetoa, jinsi ambavyo mwisho wa siku za Ibrahimu, mwisho wa Wayahudi, Wasamaria, na sasa ninii . . . mwishoni mwa wakati wa Mataifa, hapa umekuja kufanya jambo lile lile.

258 Wakati wa Kipentekoste ulianza yapata miaka arobaini, hamsini iliyopita, papa hapa kwenye Pwani ya Magharibi; jinsi walivyonena kwa lugha na kufasiri, nguvu za Mungu miongoni mwao; jinsi walivyoona wagonjwa wakiponywa, kila kitu kikitendeka, lakini sasa ishara ya mwisho imetokea kati yao. Wewe unakuja, Bwana, si muda mrefu zaidi. Hiyo ndiyo sababu ninasimama hapa usiku wa leo, Bwana, ninakuamini. Ee Mungu, wafanye watu hawa kung'ang'ania. Jalia ile—ile—ile Mbegu iliyopandwa kutia nanga ndani ya mioyo ya watu, jalia walione, jalia waliamini, jalia wawe na imani na kukuamini Wewe kwa moyo wao wote.

259 Sasa, Baba Mungu, mtindo wa kale ni kuweka mikono juu ya wagonjwa, tunajua hivyo ndivyo wanavyofanya. Mtindo wa kale ulikuwa, "Njoo madhabahuni, piga magoti na uombe." Lakini katika Biblia, ilisema, "Wote walioamini waliongezwa kanisani, wakabatizwa." Tunaamini katika mambo haya yote, bado tunafikiri yalitumikia kusudi jema, na ni vyema, tunaliamini.

260 Lakini ni kubwa zaidi sana vipi, wakati Yairo aliposema, "Njoo, uweke mkono Wako juu ya binti yangu, naye ataishi," lakini yule Mrumi, Mmataifa, alisema, "Sistahili Wewe kuja chini ya paa langu; sema tu Neno, na mtumishi wangu ataishi"?

261 Wewe ulisema, "Sijawahi kuona imani kama hiyo katika Israeli." Mungu, tusiwahi kuiachilia. Na tuweze . . . Jalia . . . Mimi . . . Jalia . . . Ninachojaribu kufanya, Mungu, kuwafanya watu waone ya kwamba Wewe ndiye Mwokozi wao, Wewe Ndiye unayeponya, Wewe Ndiye unayetoa imani. Mungu, ninaomba ya kwamba wasiwe na shaka, halafu, wakati, kama hawatatilia shaka, ndipo imani itakuja moja kwa moja ndani ya mioyo yao nao wataelewa. Jalia tukuone Wewe, Bwana.

262 Siku moja baada ya kufufuka, Kleopa na rafiki yake walikuwa njiani kuelekea Emau, wakazungumza na Yeye mchana kutwa, wala hawakumjua. Lakini jioni sana, akaingia chumbani pamoja nao, wakafunga milango. Ndipo akafanya jambo fulani jinsi tu alivyolifanya kabla ya kusulubiwa Kwake, nao wakajua kwamba hakuna mtu mwingine aliyelifanya hivyo, ndipo wakajua ni Yeye. Kwa hiyo wakarudi haraka na kuwaambia hao watu, baada ya Yeye kutoweka mbele ya macho yao, kwamba kweli Bwana amefufuka.

263 Baba Mungu, tumeweka kando jukumu letu la siku, tuko hapa usiku wa leo, chumba kimefungwa. Njoo, Bwana, fanya jambo fulani kati yetu usiku wa leo kama vile tu ulivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwako, ili sisi kwa furaha, kama walivyokuwa, turudi njiani tukisema, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, alipokuwa akizungumza nasi njiani?" Tujalie, Bwana.

264 Neno moja kutoka Kwako litathibitisha kila kitu nilichosema. Na kama nimesema kweli, nami najua, Bwana,

utathibitisha tu kweli, hutakuwa na uhusiano wowote na uwongo na makosa, unathibitisha tu ukweli, sasa Baba, ninaomba ya kwamba utathibitisha yale yaliyosemwa, kwamba ni kweli.

265 Ninajikabidhi Kwako pamoja na Neno Lako, pamoja na kusanyiko Lako la watu, na imani yao waliyoikusanya. Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba ya kwamba utajitokeza jukwaani sasa, na kuthibitisha kuwa pamoja nasi baada ya miaka elfu mbili. Wao . . . Hakuna mauti Kwake, Yeye yu hai, hata milele. Lijalie, Baba, katika Jina la Yesu. Amina.

266 Ningependa kuuliza kusanyiko, sasa, tukikaribia kufunga, kwa muda mfupi tu, nami nitawauliza, kama mtaweza, mwe na uchaji tu mwezavyo kwa kama dakika tatu. Kidogo tumechelewa kupita kiasi kufanyiza mstari wa maombi, lakini ningependa tu kuuliza swali hili kabla hatujafunga: Je, kuna mtu hapa ambaye ameshawishika kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu, nawe si Mkristo? Naweza tu kukuuliza.

267 Najua ni sawa kutoa miito mirefu sana ya madhabahuni na kadhalika, lakini haitupasi kufanya hivyo, na hadithi za huruma. Lakini usipokuja juu ya msingi wa Neno la Mungu, haileti tofauti yoyote. Unaona, wewe hupo hapo kwa vyovyote vile. Unapaswa kuja ukijua kwamba wewe ni mwenye dhambi na Yesu alikufa badala yako, nawe huna budi kuja na kuungama dhambi zako. Uko hapa . . . ? Wala sitakuita hapa juu. Nitakuuliza tu: Je, uko hapa, nawe umeshawishika kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, nawe ni mwenye dhambi unayemhitaji, waweza tu kuinua mikono yako na kusema, "Ndugu Branham, ninaamini katika maombi yako. Niombee, mimi ni mwenye dhambi, na ninataka uniombee"? Hayo tu ndiyo yote nitakayokuomba ufanye.

268 Hatutoi nyota zozote za dhahabu, na *hii*, na kuwafanya *wengi sana*, *hivi*; siamini hilo. Kama Roho Mtakatifu hawezi kukufanya ujue ya kwamba wewe ni mwenye dhambi, hakuna haja ya hata mimi kujaribu, unaona. Kwa hiyo basi, kama unaamini kwamba wewe ni mwenye dhambi, na unamhitaji Kristo, sema, "Niombee, Ndugu Branham." Inua mkono wako, nitafanya hivyo.

269 Ninyi nyote ni Wakristo? Ni Wakristo wangapi walio hapa, basi? Inueni mikono yenu, wote waliojazwa na Roho, na ni Wakristo. Mungu asifiwe. Hilo ni jema, sawa. Vema.

270 Je, kuna wagonjwa hapa basi? Inua mkono wako, uliye mgonjwa. Niko hapa kama mtumishi wa Mungu kuwatumikia. Inua mkono wako. Ukisema, "Ni—nina haja na Mungu, na ni—nina shida fulani," omba.

271 Ninyi msio na kadi za maombi sasa, ninataka tu wale wasio na kadi za maombi, maana tutatumia kadi za maombi pengine

kesho usiku, ama vyovyote vile, tukifanya hivyo, tutamwombea kila mtu aliye na kadi za maombi.

272 Ninyi msio na kadi za maombi, ninataka kuwaambia jambo fulani. Jana usiku, niliwaambia, na usiku wa leo nawaambia tena, tunajua alichofanya alipokuwa hapa duniani, kama angekuwa amerudi hapa tena, duniani usiku wa leo, katika mwili wa kawaida, angefanya jambo lile lile alilofanya wakati huo kwa sababu Yeye ni yule yule. Hiyo ni kweli? Sasa, nini kingekuwa cha zaidi ya kumwona Roho Mtakatifu akisogea katika kusanyiko hili namna hii, na kutenda kazi zile zile, na kuwathibitishia ya kwamba Yesu Kristo, Mwokozi wenu, yuko papa hapa miongoni mwenu? Jinsi linavyopaswa kuzifurahisha nafsi zenu! Jinsi mnavyopaswa kusema, "Loo, rehema!" hakuna kitu.

273 Niliona hilo likifanywa wakati mmoja, kule Afrika Kusini, wakati mmoja jukwaani, ndipo wenyeji elfu thelathini wavaao blanketi wakavunja sanamu zao ardhini na kumjia Yesu Kristo, Waislamu elfu kumi. Mnajua ni . . . Wanajisumbua kwa miaka mingi kumbadilisha mmoja wao, hao ni Wamedi na Waajemi wa kale ambao hawabadiliki. Mnaona, mnaona? Hiyo ni kweli. Bombay, India, si—sijui, sijui, sijui tu ni wangapi, usingeweza kuwahesabu, bahari tu za mikono myeusi imeinuliwa juu, kwa wakati mmoja.

274 Sasa, sisi Wapentekoste, tunaodai kubusu ukingo wa baraka za dhahabu za kikombe cha Mungu, tunawezaje kusimama kimya na kumwona Roho Mtakatifu akitenda kazi karibu nasi, Kristo Mwenyewe pamoja na Neno Lake, akithibitisha ya kwamba Yeye yuko hapa? Halafu tutulie tu, na kusema, "Vema, natamani jambo hilo litukie." Asingeweza kufanya cha zaidi.

275 Basi kumbukeni, ninawaambia, katika Jina la Bwana, kama mnaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake, katika Jina la Bwana, hamtaona ishara kubwa kuliko mnayoona sasa, kamwe hamtaiona. Sasa, iandikeni, Bibliani mwako, ukiiona, basi unipigie simu. Hii ni . . . Mnaona kitu chenu cha mwisho. Kumbukeni tu, Kanisa linaondoka. Linaingia katika Laodikia, mahali tu lilipo sasa.

276 Sasa, ombeni, aminini. Sasa, iweni tu na kicho kabisa. Haijalishi uko wapi, omba tu, iweni kimya kabisa. Mnaona, kila mmoja wenu ni roho, basi wakati huyo Roho Mtakatifu anapokuja kwenye upako, kila roho inayotembea, mnaona, unaweza kuihisi, ni wasiwasi kweli. Hiyo ndiyo sababu Yesu alimwongoza mtu mmoja nje ya mji akamponye, walikuwa wengi sana pale, mnaona. Kupita kiasi . . . Akawachukua, nyumbani kwa Yairo, na kuwatoa wote nje kabla hajamfufua binti yake, akamfufua, mnaona, kulikuwa na kutokuamini kwingi mno, walikuwa wakimcheka Yeye na kila kitu, mnaona. Huwezi kulifanya mahali ambapo pana kutokuamini, haitafaa kitu.

277 Lakini ninamwomba Mungu, usiku wa leo, athibitishe ya kwamba nimewaambia kweli, hebu na anene. Mwanadamu anaweza kunena . . . Lakini nimewaambia ukweli. Nyinyi shikilieni na kusema, "Usiku wa leo ndio wakati wangu. Maskini mhubiri huyo hanijui, hajui lolote kunihusu, lakini Mungu, Wewe ni Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, nami ninakugusa Wewe kwa imani. Ninaamini ninayo, jalia nikuguse Wewe, Bwana. Ndipo Wewe unijibu kupitia kwa Ndugu Branham na kuniambia, kama ulivyosema uliponena kwa njia ya Kristo, Mwana wa Mungu, na kumwambia, yule mwanamke aliyekuwa anatokwa na damu, na Bartimayo kipofu, na wengine wote aliowafanyia hivyo. Uniambie kwa ono." Ombeni. Iweni tu katika maombi.

278 Ni mama, anayeketi papa *hapa* nyuma, mkono wangu wa kushoto, moja kwa moja kupitia *hapa*, mwishoni wa safu. Anasumbuliwa na ugonjwa wa masikio yake. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya na kukupa afya, Mama? Wewe, unayenitazama mimi. Unaamini ataponya masikio yako na kukupa afya? Unaamini? Vema. Unayo kadi ya maombi? Huna kadi ya maombi. Huhitaji yoyote. Unaona, wewe . . . Hiyo ni, unaona, hiyo ni imani hiyo isiyojulikana uliyo nayo. Hukuwa . . . karibu hukulitarajia hilo, lakini ni . . . imani ni kitu kilichofichika. Sasa, amini tu kwa moyo wako wote, lakini usipoamini wala hutalikubali, masikio yako yatakuwa mabaya zaidi. Unaona? Sasa, kumbuka tu, kama utaamini, umegusa Kitu fulani.

279 Vipi kuhusu kupitia *hapa* chini, chini kupitia sehemu *hii* ya marefu ya kanisa? Mtu fulani ambaye ana imani, unataka kuamini, gusa tu vazi Lake. Sio mimi, haitafaa chochote, mimi ni—ni mwenye dhambi tu.

280 Huyu hapa mtu, naam, wakati uo huo alipoinamisha kichwa chake, papa *hapa*, akiomba, "Jalia iwe ni mimi, Bwana." Shida ya tumbo, hiyo ndiyo shida yako. Hatufahamiani. Je, hiyo ni kweli? Hiyo ndiyo shida yako hata hivyo, sivyo? Una ugonjwa wa mmeng'enyo, kichefuchefu tumboni na kila kitu, kuchafuka sikuzote. Umekuwa nao kwa muda mrefu. Hebu nikwambie kitu kingine, wewe si wa hapa, haya siyo makazi yako. Unatoka Portland. Amini kwa moyo wako wote sasa, unaweza kurudi, ukaponywe. Unaukubali, na kuamini ya kwamba utaponywa? Mungu akubariki. Nenda zako, amini.

281 Kuna mama aliyeketi papa hapa nyuma, ananitazama papa hapa. Ile pale ile Nu- . . . Hivi hamwezi kuiona Nuru hiyo juu ya mwanamke huyo? Angalieni *hapa*, angalieni kwa makini sana, papa *hapa*. Mnaona? Anaugua yabisi kavu. Ikiwa utaamini kwa moyo wako wote, unaweza kuponywa hiyo yabisi kavu, Bibi Trapp, kama utaamini kwa moyo wako wote. Ataukosa. Sijawahi kumwona huyo mwanamke maishani mwangu. Niliiona hii . . .

Ilikuwa karibu kukuacha, Mama, hiyo ndiyo sababu ilinibidi kuliita jina lako.

Usishangazwe na hilo, Yesu wa Nazareti alimwambia Simoni Petro kwamba yeye alikuwa nani na baba yake alikuwa nani, unaona, Yeye ni Yesu yeye yule.

282 Sasa, iwapo hatufahamiani, Mama, inua mkono wako, yule mama aliyeitwa hivi punde. Hakika, sijawahi kumwona maishani mwangu, yeye ni mwanamke aliyeketi hapo. Wewe amini.

Unaamini? Hiyo ni, inathibitisha Uwepo wa Yesu Kristo. Amina.

283 Huyu hapa mwanamke ameketi, ameketi papa *hapa*, akinitazama, kuna uvuli mweusi juu yake. Atakufa ikiwa kitu fulani hakitamsaidia, ana kansa. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya na kukupa afya? Kama unaamini, unaweza kuponywa, bali huna budi kuliamini. Amini, usiwe na shaka.

284 Ninaona hiyo kansa ikicheza, ishara hiyo, kutoka hapo, ikaenda juu ya mtu mmoja. Ameketi akinitazama. Unaamini kwa moyo wako wote, Bwana, Mungu ataiponya kansa hiyo mkononi mwako na kukupa afya? Hatufahamiani, lakini Mungu anakujua. Jambo lingine, unapaswa kuamini, wewe ni mmishenari, unayetaka kurudi Formosa tena, kuihubiri Injili. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Unajua hatufahamiani. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Bw. Graves, amini kwa moyo wako wote, unaweza kurudi, na kuponywa, upate afya. Amina.

285 Unamwamini? "Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele." Mnaamini? Ni wangapi wanaoamini kwa moyo wenu wote? Inua mkono wako. Sasa, katika Uwepo Wake, kwa nini msiwekeane mikono, mniache niwaombee hapa? Mnaona? Nayo i—itaninii . . . Inanihifadhi kidogo, inanisaidia kuendelea kire- . . . Hiyo hapo kote jengoni. Nendeni mkazungumze na watu hawa, mnajua ambapo wamekuwa, ambapo nimeninii . . . sita ama saba wa hao, ama wowote wale hapa. Waulizeni tu. Baadhi yenu katika kusanyiko, loo, kwenye roshani kule nyuma, aminini.

286 Ninampa changamoto yeyote wenu katika Jina la Yesu Kristo: Amini. Ng'ang'ania, ishikilie. Kisha ninawapa changamoto mwekeane mikono kama waaminio, na kuombeana, na kuamini ya kwamba mtapata afya, nanyi mtaipata.

287 Ninampa changamoto mtu yeyote, ambaye amekuwa mwenye dhambi, wala hajaamini, kusimama kwa miguu yako sasa na kuomba rehema, nawe utapata rehema, kama ukilimaanisha kutoka moyoni mwako, kama mlijizuia muda mfupi uliopita, ambao, kuna dazani kati yenu, mlioketi humu, ambao mlipaswa kusimama—mlipaswa kusimama kama wenye dhambi. Sasa, niambieni sijui, najua. Nami najua mumeketi

hapo bila kuamini. Ningeweza kuyaita majina yenu, mnajua hilo.

288 Ni wangapi wamekuwa mikutanoni, na kuona hilo likifanywa hapo awali? Hakika mmeona. Lakini kile inachofanya, inalidhuru kusanyiko wanalotoka. Yesu alisema, "Acha magugu na ngano zikue pamoja." Ataninii . . . Yeye ndiye atakayeyafunga. Mnaona? Lakini wewe umeketi hapa, ungewezaje kujificha? Afadhali usimame na kumkubali Kristo. Hebu nikwambie, hutawahi kuwa karibu zaidi, katika Uwepo Wake, mpaka utakapomwona Yeye uso kwa uso.

289 Kwa maana, hebu niwaambie hili, hii hapa Biblia yangu hapa mbele yangu: Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, amefufuka katika wafu, Yuko hapa, usiku wa leo, katika umbo la Roho Mtakatifu, Yeye Ndiye anayeruhusu kazi hii ifanywe.

Kumbukeni, mwaminini.

290 Wekeaneni mikono sasa, na tuombeane. Nitaziombea hizi leso kwanza. Na wakati nikiomba, uwe ukimwombea mtu uliyemwekea mikono yako, watakuwa wanakuombea.

291 Baba wa Mbinguni, ninazileta leso hizi Kwako, zinawakilisha wagonjwa. Tunafundishwa kwamba, siku moja, Israeli walikuwa kwenye wajibu wao, wakienda zao kwenye nchi ya ahadi, nayo Bahari ya Shamu ikawazuia papo hapo. Israeli, wakiwa katika wajibu wao, wakizifuata amri za Mungu, ndipo Bahari ya Shamu ikawazuia moja kwa moja, kuwakatilia mbali na ile ahadi. Mwandishi mmoja alisema ya kwamba Mungu alichungulia chini, kupitia hiyo Nguzo ya Moto, nayo bahari ikaogopa, nayo ikajirudisha nyuma, na kutengeneza njia kavu Israeli wapate kuvuka kuingia kwenye nchi ya ahadi.

292 Wewe ungali ni Mungu yeye yule, usiku wa leo. Ugonjwa na maradhi yamewakatilia mbali watu kutoka kwa . . . wanaotembea moja kwa moja katika wajibu wao, Nawe ulisema, "Zaidi ya yote, nataka usitawi katika afya yako," na naomba Mungu, aliyetoa hiyo ahadi, asiangalie tu kupitia ile Nguzo ya Moto, bali kupitia Damu ya Mwanawe Mwenyewe, Yesu Kristo, pia jalia magonjwa hayo yaogope na kurudi nyuma kutoka kwa watu. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu Kristo.

293 Sasa, Shetani, wewe ambaye umewafunga watu na kuwazuia miaka hii yote, ukawaweka wamefungwa katika magonjwa, tunakuja kama wawakilishi wa Kristo, nasi tunakuapisha Kwake, Yeye aliyetupa mamlaka ya kufanya hivyo, waache hao watu. Toka ndani yao, katika Jina la Yesu Kristo.

294 Jalia nguvu zilizomfufua Kristo kutoka kaburini zivunje kila shaka juu ya mioyo ya watu, ili wapate kupokea uponyaji wao, sasa hivi, katika Jina la Yesu Kristo.

295 Wote wanaoamini, simameni kwa miguu yenu, katika Jina la Yesu Kristo, na kukubali uponyaji wenu, bila kujali una shida gani. Amina. *Nitamsifu*; *Nitamsifu.*

Ni . . .

Nitamsifu! Hebu tumpe Yeye sifa, kila mtu.

. . . msifu, nitamsifu,
Ee, msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
Loo, mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha na kuondolea mbali kila waa.

296 Sasa, ili kuondoa ubaridi, na pingu kukatika karibu nasi, mizuka kuondolewa . . . Hiyo ndiyo . . . Kuna nini, enyi watu? Je, hamtambui ya kwamba tunaingia, baada ya huo ujumbe, katika roho ya kuabudu? Hebu na tumwinulie Mungu mikono yetu, na kumwabudu, na kusema, "Bwana asifiwe. Mungu asifiwe. Ashukuriwe Baba, anayetupa Mwana wa Mungu, aliyefufuka katika wafu, aliye hai hata milele; Alfa, Omega; Mwanzo na Mwisho, Ua la Uwandani; Ninyoro ya Bondeni; Nyota ya Asubuhi; Yeye aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja; Shina na Mzao wa Daudi.

297 Jinsi tunavyokusifu, Mungu Mwenyezi, kwa uwepo Wako kila mahali, kwa ajili ya Wewe kutuzuru, usiku wa leo, kwa ajili ya nguvu za kufufuka Kwako, kwa hakikisho la wokovu, kwa dhihirisho Lako kuu la Neno Lako katika siku hizi za mwisho ulizoahidi kwamba ungefanya! Mbele ya ukosoaji, na taratibu, na kila kitu, Wewe ungali unabaki kuwa Mungu, Mungu yeye yule jana, leo, na hata milele. Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili yake, Baba! Amina. Amina.

298 Loo, hivi hamjisikii vizuri? Semeni, "Bwana asifiwe." Loo, hiyo haisikiki kama Pentekoste kwangu. "Bwana asifiwe!" Hiyo inasikika bora zaidi. "Amina." "Utukufu kwa Mungu." "Nampenda Yesu." "Mungu asifiwe." Amina.

Nitamsifu,

Hebu tuinue mikono yetu sasa na tuuimbe.

Na . . .

Ufanye usikike.

. . . msifuni,
Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
Loo, mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa maana Damu Yake inaweza kuosha na kuondolea mbali kila doa.

299 Unampenda? Sema, "Amina." Unampenda jirani yako? Sema, "Amina." Sasa, hebu tupeane mikono na mtu . . . mtu aliye

karibu nawe, mbele yako. Simameni tu kimya, peana mikono tu, mtu aliye karibu nawe, mkisema, "Bwana asifiwe. Bwana asifiwe." Bwana asifiwe. Bwana asifiwe. Mungu asifiwe. Bwana asifiwe. Bwana asifiwe. Bwana asifiwe.

Hivi hamjisikii vizuri? Amina. Sasa, hebu tuuimbe tena.

Nitamsifu . . .

Inueni mikono yenu.

. . . nitamsifu,

Kubwa sana sasa.

Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili
ya wenye dhambi;
Loo, mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha na kuondolea
mbali kila waa.

300 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa, kwa muda kidogo. Je, mnaamini katika uamsho wa mtindo wa kale? Je, mnaamini katika uwezo wa Mungu? Je, mnaamini katika dini ya wakati wa kale? Loo, haipaki chokaa, bali huosha ikawa nyeupe na ikawa safi kama theluji. Unaamini hilo kwa moyo wako wote? Tuombe sana sasa Mungu aanzishe moja ya miamsho hiyo.

301 Hebu tuweke mabega yetu, marafiki, hatuna budi kuendelea kusukuma, kusukuma. Hebu tung'ang'anie. Lazima tuone hili likitokea, lazima litokee, lazima tufanye hivyo.

302 Sasa, wakati mmeinamisha vichwa vyenu, nitamleta mchungaji sasa, mwenyekiti wa mkutano, hapa jukwaani, na kumruhusu aipeleke ibada kwenye chochote . . .

62-0719E Anayeng'ang'ania
National Guard Armory
Salem, Oregon Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org